# MAUDHUI YANAVYOIMARISHWA NA FANI KATIKA RIWAYA YA *NGUVU YA SALA* YA K.W WAMITILA

**NA**

**NJUGUNA, SAMUEL MUIRURI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**2016**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

______________________________ ____________________

NJUGUNA, SAMUEL MUIRURI. Tarehe

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi wa kazi aliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi

________________________ ___________________

DKT.EVANS MBUTHIA. Tarehe

(Mtahini)

## TABARUKU

Nitabarukia tasnifu hii mke wangu Susan Muiruri na watoto wangu wapendwa Brian na Betty kwa kunitia moyo katika masomo yangu muda huu wote nimekuwa chuoni.

## SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani kwa Dkt Evans Mbuthia kwa usimamizi wake mzuri ambao umeniwezesha kuandika tasnifu hii. Napenda kuwashukuru wahadhiri wangu katika idara ya Kiswahili, Profesa John Habwe, Profesa Kyallo W. Wamitila, Prof.Iribe Mwangi, Bw. Basilio Mungania na Dkt George Mweri kwa kunielekeza na kunifunulia ulimwengu wa usomi.

Shukrani nyingine ziwaendee wanafunzi wenzangu, Lincoln Nyaga, Mary Apopo, Josphine Mbula, Andrew Watuha, Danson Ngunjiri, Joyce Murage, Joyce Karinge, Alex Kinyua, Oruga Owanda, Simon Wanjala na Peter Mburu kwa ushirikiano wao.

Shukrani zaidi ziwaendee wafanyakazi wote wa maktaba kuu ya Chuo Kikuu cha Nairobi kwa huduma yao ambayo haitasahaulika.Mwisho ningependa kutoa shukrani kwa Florence Otiende kwa kuipiga taipu kazi hii kwa uangalifu mkubwa

## ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

**TUKI** Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

**uk.** Ukurasa

## IKISIRI

Kazi yetu imechunguza vipengele vya fani. Tulifafanua dhana ya fani kwa kusema kuwa, fani ni vipengele vya kisanaa katika kazi ya fasihi. Aidha, fani ni jinsi ambavyo msanii hufinyanga kazi yake ili msomaji apate ujumbe wake kwa njia iliyo nzuri. Kazi yetu imetumia nadharia ya umuundo kuchambua vipengele vya fani. Kazi hii imechunguza vipengele vifuatavyo; Msuko, mandhari na wahusika. Tumechunguza namna mandhari mbalimbali yanavyowaathiri wahusika na kubadilisha misimamo yao kuhusu mambo tofauti.Pia tumechunguza namna mwandishi aliyoendeleza maudhui yake kwa kutumia misuko ya aina mbali mbali. Aidha tumechunguza namna wahusika tofauti walivyotumiwa kukuza maudhui ya kazi hii. Kutokana na uchuguzi huu imebainika kuwa maudhui huimarishwa na mwandishi anapotumia vipengele tofauti vya fani kwa ustadi ili kukuza ujumbe wake.

Hii ni kutokana na kweli kwamba mambo ambayo huelezwa kikawaida hutiliwa mkazo na mbinu za kifani zilizoteuliwa na mwandishi na kwa kufanya hivyo ujumi huimarika,kazi hupata mvuto na hatimaye maudhui hueleweka vyema na kwa ukamilifu.

**YALIYOMO** **UKURASA**

UNGAMO ........................................ ii

TABARUKU ........................................ iii

SHUKRANI ........................................ iv

ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ........................................ v

IKISIRI ........................................ vi

YALIYOMO ........................................ vii

**SURA YA KWANZA**

1.1 Utangulizi ........................................ 1

1.2 Tatizo la Utafiti ........................................ 2

1.3 Madhumuni ya Utafiti ........................................ 2

1.4 Maswali ya utafiti ........................................ 2

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ........................................ 3

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........................................ 3

1.7 Msingi wa Kinadharia ........................................ 3

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili ........................................ 6

1.9 Njia za Utafiti ........................................ 8

**SURA YA PILI**

**UHAKIKI WA FANI KATIKA NGUVU YA SALA**

2.1 Utangulizi ........................................ 9

2.2 Msuko Mkuu ........................................ 9

2.3 Visuko ........................................ 14

2.6 Hitimisho ........................................ 22

**SURA YA TATU**

**MANDHARI KATIKA NGUVU YA SALA**

3.1 Utangulizi ....................................................................................................................24

3.2 Mandhari ya Mjini ..........................................................................................................24

3.3 Mandhari ya Mashambani. ..............................................................................................27

3.4 Mandhari ya shuleni ........................................................................................................37

3.5 Hitimisho .........................................................................................................................40

**SURA YA NNE**

**SWALA LA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA *NGUVU YA SALA***

4.1 Utangulizi. .......................................................................................................................42

4.2 Wahusika wakuu katika *Nguvu ya Sala* ...........................................................................42

4.2.1 Susan Nzisa......................................................................................................................43

4.2.2 Richard Ngunze ..............................................................................................................45

4.3. Wahusika wadogo............................................................................................................47

4.3.1 Mary Kasiva ....................................................................................................................48

4.3.2. Roselyn ...........................................................................................................................49

4.3.3 Bethsheba.........................................................................................................................50

4.3.4 Octavian Birundu ............................................................................................................51

4.3.5 Sista Emily.......................................................................................................................53

4.3.6 Redemta na Jacquiline .....................................................................................................54

4.3.7 Manyara na Mkewe .........................................................................................................55

4.3.8 Rose Mafali......................................................................................................................56

4.4 Hitimisho .........................................................................................................................57

**SURA YA TANO**

**MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.1 Utangulizi ..... 59

5.2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti ..... 59

5.3 Hitimisho ..... 64

5.4 Mapendekezo ..... 64

MAREJELEO ..... 65

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Fani ni dhana muhimu sana katika fasihi. Wamitila (2008) anasema kuwa fani ni jumla ya nyenzo zinazotumika kuwasilisha kazi yoyote ya fasihi. Anaongeza kwamba mawazo ya mwandishi wa kazi yoyote ya fasihi huwa katika uchi wake hadi pale fani inapotumika na kuyavisha nguo mawazo hayo ili yaweze kuwasilishika. Hivi kwamba fani pamoja na maudhui hutegemeana na kukamilishana.

Wataalam wa fasihi kwa wakati mmoja wamefananisha uhusiano uliopo kati ya fani na vipengee vingine vya fasihi kama mfumo. Hivi kwamba katika mfumo huu hauwezi kukamilika pasi na sehemu zote kuwepo.

Mawazo ya Wamitila yameungwa mkono na Mbatiah (2001) anaposema kuwa fani katika kazi ya fasihi hujenga kiunzi cha kubebea ujumbe na maana mahususi. Mtaalamu huyu ana maana kuwa hapatakuwa na ujumbe katika kazi ya fasihi iwapo fani itakosekana katika kazi hiyo. Hivyo basi inamlazimu msanii yeyote wa kazi ya fasihi awe mweledi katika kufinyanga nyenzo hii ya fani ili kuwasilisha kazi yake vyema.

Vipengele vya fani tulivyovishughulikia ni; msuko, mandhari na wahusika. Vipengele vya fani ni vingi lakini tulishughulikia hivi vitatu katika kazi yetu. Kwa vyovyote vile, fani ni dhana ambayo ni muhumu katika kufanikisha kazi yoyote ya fasihi. Aidha fani hutumika kwa njia tofauti kutegemea utanzu husika.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Kila mwandishi ana uhuru wa kutumia vipengee vya fani kama atakavyo. Jambo hili hufanya kazi ya fasihi kuwa tofauti kutoka msanii mmoja hadi mwingine.hata tofauti za kitanzu huwafanya waandishi mitindo inayofaa kwa kutegemea utanzu unaohusika.

Katika *Nguvu Ya Sala* (2003), mwandishi anatumia vipengele anuwai vya fani katika uwasilishaji wake wa ujumbe. Anatumia wahusika wa aina tofauti kama vile wazazi na watoto wao pamoja na wahusika wengine wanaotagusana nao katika mandhari tofauti. Aidha ametumia mandhari kama vile ya mjini, mashambani na hata shuleni. Isitoshe ametumia kipengele cha msuko. Katika kipengele hiki kuna msuko mkuu pamoja na misuko mingine midogo midogo inayojenga taharuki ya kudumu riwayani.

Kwa pamoja vipengee hivi vinaimarisha ujumbe katika kazi hii kama inavyoidhihirishwa katika tasnifu hii. Ufundi unaodhihirika katika uwasilishaji wa ujumbe unaimarisha kazi yenyewe na kuipatia mvuto kwa msomaji.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni;

i. Kuchunguza jinsi mwandishi alivyotumia misuko anuwai katika kukuza kazi yake.
ii. Kuchunguza namna mandhari tofauti yanavyoathiri mitazamo ya wahusika katika riwaya.
iii. Kuchunguza nafasi ya wahusika mbali mbali katika kuendeleza maudhui katika riwaya.

## 1.4 Maswali ya utafiti

Utafiti wetu utaongozwa na maswali yafuatayo:

i. Je mwandishi ametumia kwa njia gani misuko tofauti katika  kukuza kazi yake?
ii. Je mwandishi ametumia mandhari kwa namna gani katika kusawiri mielekeo ya wahusika wake?
iii. Je wahusika tofauti wana mchango upi katika ukuzaji wa maudhui katika riwaya ya *Nguvu Ya Sala?*

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Tumechagua mada hii kwa sababu mwandishi amedhihirisha utaalamu wa hali ya juu katika matumizi ya fani. Mwandishi huyu ametumia misuko anuwai na mandhari tofauti tofauti kwa njia ambayo inakuza kisa chake kwa njia inayovutia. Pia mwandishi amewatumia wahusika wa aina tofauti tofauti na kuwapa majukumu mbali mbali ili kukuza kisa chake.Riwaya hii pia haijahakikiwa katika mtazamo tuliyoutumia.

## 1.6 Upeo na Mipaka ya  Utafiti

Tasnifu yetu ilichambua vipengele vya fani katika riwaya ya *Nguvu Ya Sala* ya K.W. Wamitila. Vipengele hivi ni;msuko, mandhari na wahusika.

Uchambuzi wetu umeongozwa na nadharia ya umuundo ambayo tumeitumia kuonyesha  namna vipengele husika vilivyotumika katika kuboresha maudhui katika kazi hii.

## 1.7 Msingi wa Kinadharia

Wamitila (2002) anatueleza kuwa umuundo unahusishwa na wanaisimu wa shule ya Prague. Wanaisimu hawa walihusika na urasimu wa Kirusi.

Kwa hivyo shule ya isimu ya Prague ilishughulikia urasimu.Waasisi wa nadharia ya urasimu ni kama vile Roman Jakobson. Viktor Sklovij. Juri Tynjanov na wengineo.

Nadharia ya urasimu ilizuka mwanzoni mwa karne ya ishirini. Makundi mawilii yanayohusishwa na mwanzo huu wa urasimu ni kama vile kundi la wanaisimu la Moscow na kundi la uchunguzi wa lugha ya kishairi. Hata hivyo makundi haya mawili yalitofautiana katika miundo ya kiujumi.

Wananadharia hawa walichochewa kuitazama fasihi kama sanaa ya maneno kuliko kama akisicho la jamii.Walihusika sana na kazi maalum za kifasihi wala sio chimbuko wala athari zake kwa wanaosoma fasihi. Hamu kuu ya wataalamu hawa ilikuwa kubainisha sifa za kuitambulisha fasihi na kuweka mipaka kati ya fasihi na taaluma nyinginezo kama saikolojia,wasifu historia na taaluma nyinginezo. Waasisi hawa walisisitiza kuwa uandishi wa kibunifu unaotambulishwa na msisitizo wa njia za kiwasilishaji. Wanaisimu hawa wanasema kuwa fasihi inajinasibisha na vitu ambavyo vinakuwa vya kawaida au kidesturi katika maisha yetu na kuvifanya vionekane kama vya kigeni.

Mbatiah (2001) anaunga mkono wazo hili kwa kusema kuwa, umuundo unaangaliwa na wahakiki wengi kana nadharia iliyotokana na ufani au urasmi. Waasisi wa nadharia ya umuundo walijishughulisha na muundo wa ndani wa kazi ya kifasihi.

Mwangi (2005), katika tasnifu yake akifafanua mawazo ya Culler anaeleza kuwa lazima uhakiki wa kimuundo uweze kubainisha mifumo ya kindani ya sanaa. Mifumo hii inaviwezesha viungo vyake vya fani kuwa na taathira katika kazi ya fasihi. Hivyo fasihi inapohakikiwa yapaswa kuhakikiwa kama sayansi. Yaani lazima ijisimamie kwa viungo vyake bila kushughulikia maswala yaliyo nje yake.

Mchango wa Wamitila (2002) katika mawazo haya ya uhakiki ni kuwa, mhakiki hawezi kufanikisha kazi yake bila ya kuutumia mkabala wa kimethodolojia. Uhakiki wa kimuundo ni ufafanuzi wala sio kufasiri kazi za kifasihi. Mhakiki wa kimuundo huangalia sehemu mbalimbali za kifasihi na kuonyesha jinsi zinavyounda muundo mzima. Mawazo ya Saussure kama tunavyoelezwa na Wamitila ni kuwa, kuna matendo ya kiusemi yaani Parole na mfumo mpana wa lugha au Langue. Dhana ya Langue ina maana kuwa lugha hujengwa na vipengele mbalimbali vya lugha hiyo kama vile Semantiki mofolojia na vipengele vinginevyo. Wazo hili linahusiana na jinsi ambavyo fasihi ina vipengele vyake kama vile wahusika. Ploti, lugha na nyinginezo. Vipengele hivi viwe vya lugha yaani vya Langue na Parole ama vya fasihi huwa ni viungo vya ndani. Isitoshe vipengele hivyo huchunguzwa kisayansi. Aidha mtunzi au mtumiaji hutumia vipengele hivi kufuata kaida za lugha au fasihi.

Dhana ya Parole huhusiana na fasihi kwa namna fasihi inavyoandikwa. Mtunzi anaposimulia fasihi huwa kama kutumia lugha yake kiutendaji. Tunapata ujumbe wake baada ya mtunzi kubuni na kuandika kazi yake. Uandishi huu ni tendo la kibinafsi na hivyo una upekee wa aina fulani. Ndipo tunapata kuwa fasihi huwasilisha mawazo na ujumbe tofauti kutoka mtunzi mmoja hadi mwingine. Hivi ndivyo ilivyo katika usemaji. Kila mtu ana upekee wa usemaji na huleta dhana ya ubinafsi. Haya mawazo yanatokana namaana ya istlahi ya Parole. Ndipo tukasema mawazo ya Saussure yana mchango mkubwa katika nadharia ya umuundo. Kwenye muundo wa riwaya ndimo mna mshikamano wa hadithi mzima na hiyo kuhakiki kimuundo ndiyo njia ya kuona mfuatano na muoano wa matukio yote. Forster (1927) Anatazama mambo kimuundo kutokana na maelezo yake kuwa vitendo katika riwaya huwa na sifa ya kusababishana. Maelezo yake yanatuelekeza kuona kuwa kadhia tofauti katika riwaya huwa na uhusiano kwa kuwa kila mojawapo huwa ni kama kipande cha nyuzi zinazoshona kamba.

Kuangalia riwaya kimuundo ni kuyachunguza mawazo ya mwandishi yalivyojengwa na namna alivyoweza kutumia vigezo muhimu vya lugha. Aidha kuangalia kimuundo ni kujaribu kukaribia mwandishi katika kazi yake. Hizi ndizo baadhi ya sababu zilizotufanya kuchagua nadharia ya umuundo.

### 1.8 Yaliyondikwa Kuhusu Somo Hili

Mlacha (1991) amechangia pakubwa kwa kueleza maana ya riwaya kwamba ni hadithi zenye matukio mapana. Ametufahamisha kuwa ujumbe wa riwaya hukuzwa na kuendelezwa na vigezo ambavyo ni vipengele vya fani. Ametaja wahusika, msuko na vinginezo. Aidha amesema kuwa matukio lazima yaunganishwe vizuri ili kutoa picha ya tukio linaloonyesha kuwa linaweza kutokea au lililokwisha kutokea. Aidha ametueleza kuhusu kipengele cha wahusika kwa upana. Ameeleza mhusika mkuu kwa njia nzuri. Yaani sifa za mhusika mkuu ambazo zimetusaidia kutambua mhusika huyu kwa njia rahisi. Amewaainisha wahusika vizuri na huu umekuwa msaada mkubwa kwetu.

Musyoka (1996) katika tasnifu yake, amehakiki vipengele vya fani za fasihi kama vile ploti, wahusika na matumizi ya lugha. Mtaalam huyu akifafanua maana ya fani anasema kuwa, fani ni vile vipengele vya kisanaa ambavyo kwa pamoja hujenga umbo la kisanaa. Kazi ya fasihi hujengwa kutokana na uteuzi wa vipengele vya fani vya kibinafsi vilivyotumiwa na mtunzi ambaye pia huwa na uwasilishaji wa kipekee na wenye kutambulisha ubinafsi wa uumbuji wake. Musyoka anachokieleza ni kuwa matumizi ya fani katika kazi ya kisanaa ni muhimu katika kazi ya fasihi.

Jambo jingine la kukumbukwa ni kuwa, kila msanii ana mtindo wake wa kutumia fani hizi. Wakati mwingine mtindo huu wa kibinafsi humtabulisha kati ya watunzi wengine. Kulingana na mtaalamu huyu fani ni mjumuiko wa vipengele vya kisanaa ambavyo huchangia katika ukamilifu wa kazi maalum.

Njia hizi za uwasilishaji tunaziita mtindo wa usanii. Aidha,fani huwa na uamilifu wakuunda maudhui ya kazi husika. Yaani kuna uhusiano kwenye kazi ya fasihi. Kazi hii ilitupatia maelezo maalum yaliyotusaidia katika utafiti wetu.Tofauti tuliyoipata ni kuwa, Musyoka alishughulikia tamthilia ilhali utafiti huu unahusu riwaya.

Kazi ya Mbatiah (2001) imekuwa muhimu sana kwetu. Kama mhakiki wa fasihi ametupatia maelezo mazuri ya fani. Amesema fani ni jumla ya vipengele vinavyojenga kazi ya fasihi. Tumeelewa kuwa vipengele hivi ndivyo mtunzi anavyotumia kuunda kazi yake. Wazo hili limetufanya kuchunguza vipengele hivi ili kupata athari yake kwa mtunzi na kwa msomaji. Tumefahamu kuwa vipengele hivi hutumika pamoja kwa njia mahsusi katika kila kazi ya kubuni kwa kutegemea mwandishi au utanzu.

Wamitila (2002) ametoa maelezo kuhusu maana ya riwaya. Aidha ametoa maelezo ya vipengele vya fani tunavyoshughulikia kama vile wahusika, ploti au msuko. Ametoa maana ya msuko vizuri sana na ameainisha wahusika na kutupatia sifa zao jambo ambalo limetufanya kuelewa kipengele hiki vizuri. Aidha tunapata maelezo mengine ya nadharia ya umuundo.

Tumepata mawazo kuhusu mwanzo wa nadharia hii pamoja na maendeleo yake. Pia amewataja waasisi wa dhana hizina kwa hivyo kazi hii ilitufaa sana.

Too (2011) katika tasnifu yake ya uzamifu, amefanya uchunguzi wa kifasihi wa baadhi ya fani za fasihi katika kazi ya *Nguzo Mama*. Ametumia nadharia ya umuundo na simioteki.

Kuna tofauti kubwa na utafiti wetu kwa maana alishughulikia tamthilia ambayo ni tofauti na kazi yetu ya riwaya. Hata hivyo, sehemu aliyofafanua ilichangia ufahamu wetu wa dhana ya fani.

Tambasi (2011) katika tasnifu yake ya M.A alihakiki fani akitumia nadharia ya umuundo. Tofauti ilioko na kazi yetu ni kuwa yeye alifanya uhakiki wake katika kazi ya *Tambuka* ambao ni utanzu wa shairi. Kazi yake ilitufaa sana kwa maana dhana ya fani aliyoeleza ilitupatia mwangaza kuhusu fani za kifasihi.

**1.9 Njia za Utafiti**

Utafiti wetu ulikuwa kimsingi ni wa maktabani. Tulisoma tasnifu tofauti zinazolenga fani na nadharia ya umuundo ili tuweze kuelewa namna nadharia hii inavyoweza kutumika. Pia tulisoma kwa makini kuhusu nadharia ya umuundo ili kufahamu namna ya kuitumia katika uchanganuzi wetu wa *Nguvu Ya Sala*. Aidha tulisoma riwaya ya *Nguvu Ya Sala* kwa makini ili tuweze kutambua namna vipengele vya fani hasa vile vya wahusika, mandhari na msuko vinavyotumiwa na mwandishi ili kukuza ujumbe wake.

# SURA YA PILI

# UHAKIKI WA FANI KATIKA NGUVU YA SALA

Sehemu hii tunashughulikia kipengele cha msuko ambacho ni mojawapo wa vipengele muhimu vya fani. Misuko katika riwaya hutumika kukuza maudhui katika ya kazi ya riwaya. Riwaya ya *Nguvu Ya Sala* ina msuko mkuu pia visuko vidogo. Visuko hivi kwa pamoja hujenga msuko mkuu ambapo maudhui ya kazi nzima hujengeka.

## 2.1 Utangulizi

Wamitila ametumia msuko sahili na msuko wa kioo. Msomaji anakutana na Richard akiwa mtu mzima na baadaye kwa kutumia mbinu rejeshi. Tunafahamishwa kuhusu maisha yake ya hapo awali. Maisha ya familia yake wakiwemo mke wake Kasiva na binti zake Susan, Roselyn, Jacquiline na Redemta yanasimuliwa kwa njia ya moja kwa moja.

## 2.2 Msuko Mkuu

Msuko mkuu unasimulia juu ya Richard Ngunze na Susan Nzisa. Richard ana msimamo unaotiliwa shaka na bintiye. Richard alipenda familia yake iwe kielelezo cha kuigwa na wengine kimaadili kutokana na mafunzo ya Biblia. Haikuwa mapenzi ya Richard watoto wake kuwa na mazoea ya kucheza na wototo wengine ambao hawakuwa Wakristo. Hadithi inatufahamisha kuwa watoto walishangaa wala hawakuelewa sababu ya msimamo huu. Richard alizoea kuwapiga watoto wake kwa kushiriki michezo na wenzao ambao hawakuzingatia ukristo. Alisisitiza sana watoto wake kutochelewa nje na kuzingatia nguvu zilizopatikana katika sala. Alichukua muda mrefu kuwafunza sala ikiwa ni pamoja na mafundisho mengine ya kidini.

Mwandishi anatufahamisha kuwa hata wazee wa kijiji walimwelewa katika misimamo yake ambapo wengine walimpenda ilhali wengine walimchukia. Msimamo wake wa kidini ulimfanya asione haja hata kidogo ya kufuata itikadi za kitamanduni. Richard aliuukata mkuyu uliokuwa karibu na kwake jambo ambalo wanakijiji waliona kama kukaidi au kupuuza itikadi na imani zao. Susan aliogopa kuuliza baba yake maswali kwa sababu alikuwa amekatazwa tabia hii kwa kuwa ingempelekea kuwa na umbea. Kulingana na Richard Ngunze umbea haukuwa mzuri kwa mkristo. Susan alimwogopa baba yake sana.

Hili tunalipata wakati Susan alipoandamana na wenzake baada ya kumaliza mtihani wa shule ya msingi. Alipofahamu kuwa baba yake alikuwa akiuliza alipokuwa, alihofia angemezwa mzimamzima. Susan alijua lolote lingetokea. Siku hiyo alipata kichapo kikali kutoka kwa babake. Richard Ngunze alipenda sana watoto wasishiriki tabia mbaya za watoto wengine.

Tunaambiwa kila mara alipomtuma mmoja wa watoto wake angehakikisha Redemta mtoto wake aliyekuwa mdogo ameandamana naye. Redemta alipendwa sana na babake. Alimpenda kwa sababu alimwona mwenye tabia nzuri kuliko dada zake wote. Kusudi kuu la kumtaka Redemta kufanya hivyo ilikuwa kumweleza yote yaliyotendeka njiani. Hili linajitokeza wakati Susan alipokwenda kwa rafikiye James. Walipochelewa kurudi, Richard alimwita Redemta kando na kutaka kujua sababu yao kuchelewa. Redemta alimfahamisha babake kuwa Susan na mwenzake James waliongea lugha ya Kiingereza.

Susan haelewi kosa la kutumia lugha ya Kiingereza. Susan alionywa dhidi ya tabia ile. Susan hakuelewa kama shida ilikuwa kuchelewa njiani ama kuongea lugha ya kiingereza na James. Susan anaona baba yake akiwa na udhaifu wa aina fulani. Alimwona katili kwa kuwanyima dada zake nafasi ya kushiriki michezo na wenzao hasa wa marika yao.

Baada ya kumaliza shule ya upili yaani kufanya mtihani wa mwisho, Susan alienda nyumbani moja kwa moja. Hakutaka kushiriki sherehe kama mwenzake Bethsheba. Susan hangefanya uamuzi mwingine kwa sababu huenda hakutaka kufanya kinyume na jinsi mapenzi ya babake yangekuwa. Susan alipokuwa anaelekea nyumbani saa zilienda hivi kwamba aliwasili saa moja na robo usiku. Alibahatika kusindikizwa na Cedric Mwambe. Mtu huyu walikutana garini na wakawa wanasafiri pamoja. Susan hakutaka Cedric kufika nyumbani ili kwamba asionekane na baba yake. Susan hakupenda kuaibishwa mbele ya Cedric.

Tunaambiwa kuwa, Nguze angemdhania Cedric kuwa mpenzi wake Susan hivyo akamrudishia Susan sanduku lake. Kwa hivyo, ilimbidi Susan kubeba saduku lake mkono mmoja na mfuko kuuning'iniza upande wa kulia. Haya yote yanatufahamisha kuwa, bado katika kiwango hiki Susan angali anamwogopa baba yake.

Hata ingawa Susan alikuwa katika kidato cha nne, babake alimwona bado mtoto aliyehitaji kutunzwa. Susan alipofika nyumbani, mazungumzo aliyoyapata kati ya babake, mamake na babake Bethsheba yalikuwa ya kidini kuonyesha dhahiri kuwa bado mawazo ya kidini yalitawala mji ule. Maneno kama vile, hizi ni siku za mwisho na yule atakayevumilia mpaka mwisho ndiye atakayeuona ufalme wa mbingu.

Tunagundua kuwa Susan aliathiriwa na mafundisho ya Biblia kama walivyofunzwa na baba nyumbani. Akiwa chuoni baada ya kutembelewa na kijana fulani alikiri kuwa yeye alikuwa Mkristo.

Susan alipogundua kijana yule alidharau Biblia, aliona kama tusi kubwa na ikiwa babake angekuwa karibu na kusikia yale angemwomba Mungu alete adhabu mara moja kama ya Sodom na Gomorah.

Kwa hivyo hata ingawa Susan anauona msimamo wa babake wa kikriso kama kikwazo kwenye uhuru katika maisha yake, mafundisho aliyoyasikia babake akiyafundisha yalimwingia akilini. Susan akiwa chuoni aliweza kuona mengi. Baadhi ya mambo haya, yalimfanya kuona maisha kwa uazi. Kati ya mambo aliyoyaona ni mgomo chuoni wanafunzi wakipinga sera zilizochangia gharama ya masomo. Alishuhudia mwanamke mmoja aliyepokonywa kibeti chake na mvulana mmoja na hata alipopiga kamsa hamkuwa na yeyote wa kumsaidia. Watu walibaki wakimwangalia tu.

Mwanzoni vituko hivi vilimtia Susan wasiwasi kiasi cha kufanya maombi. Lakini baadaye alikuja kuzoea mambo haya na kukubali uhalisi wa mambo. Alionelea kuwa kile kilichohitajika ni mageuzi katika jamii na sio nguvu ya maombi kama alivyofunzwa na wazazi wake. Kwanzia hapa ndipo tunapata Susan akiwa na mawazo tofauti ya kidini kama babake bado alivyoshikilia kuwa kila jambo lilihitaji nguvu ya maombi.

Maisha ya Susan chuoni yalibadilisha mtazamo wake wa mambo. Tunamkuta akimkosoa babake kwa kumfukuza mnuna wake Roselyn baada ya kufukuzwa shuleni baada ya kupata mimba. Susan alipata msukumo mkubwa wa kukabiliana na babake huku akimpasulia yaliyomkaa moyoni kwa muda mrefu. Susan hajioni mtoto tena. Alikuwa tayari kumtetea mnuna wake.Tukio hili lilimshangaza mamake. Kipindi hiki cha mabishano kati ya Susan na babake kilishangaza hata wadogo wake.

Richard mwenyewe alishangazwa na tukio hili pia. Alikuja juu na midomo yake ikaanza kumchezacheza. Richard alipatwa na hasira nyingi. Susan aliendelea kumkosoa babake kwa kumfukuza Roselyn akieleza kuwa kitendo hiki hakikusuluhisha lolote wala chochote.

Susan alisisitiza kuwa kama kulikuwa na makosa yoyote, yalikuwemo kwenye malezi waliyopata kutoka kwa wazazi wao. Susan alitoa tetezi kuwa, Richard alikazania mafundisho ya Biblia yafuatwe bila kueleza hali halisi katika ulimwengu. Richard na mkewe walitakiwa kuelewa huo ulikuwa wakati tofauti. Kulingana na Susan wazazi wake walifaa waelewe umuhimu wa kuwalea kulingana na wakati wao.

Richard alisisitiza kuwa haikuwa halali kupingana na bintiye lakini hilo halikumtisha Susan. Susan anashangaa wanawake wamekuwa wakidharauliwa. Susan anachukulia kuwa mateso yote ambayo walikuwa wakipitia ni kwa sababu walikuwa jinsia ya kike. Susan anasema wakati umefika mambo yabadilike usiwe wakati wa kupokea maagizo tu bila ya kujua sababu na kiini chake. Susan analalamika kuwa binadamu huhitaji uhuru na uhuru ukikosa kupatikana kuna haki ya kuasi. Susan analalamikia uongozi mkali wa baba yake. Tetezi zake ni kuwa ikiwa kulikuwa na haja ya kutumia nguvu ya sala, kwa nini Roselyn alipopata shida hawakutumia nguvu hii. Susan anawauliza kwa nini hawakukumbuka kutumia nguvu na sala.

Tetezi hizi zilimfika Richard mwisho akainuka juu kama morani wa kimasai huku akidai kuwa hajawahi kutolewa maneno na mwanamke. Susan alikuwa tayari kukabiliana na babake bila uwoga. Susan alilalamikia upofu ulioletwa na imani kwani huu ulikuwa wakati mwingine. Susan aliuona upofu wa kumfukuza mtoto nyumbani kwa misingi ya imani. Alikiri kuwa watu walikosa imani na dini ya Richard.

Imani inayovunja mji haikufaa Susan alilalamika. Katika mwisho wa tukio hili tunamwona Richard akikosa la kufanya kwani anaonekana akilegezwa na maneno ya Susan. Msuko huu ambao tumeshughulikia ndio msuko mkuu. Msuko huu umewahusisha wahusika wakuu ambao wamechukua nafasi kubwa. Tukio hili linaeleza mgogoro mkubwa kati ya Richard na bintiye.

Msuko huu unamsawiri Susan akitaka kuwa na uhuru lakini anapata kizuizi ambacho kilikuwa ni baba yake. Sifa hii ya mgogoro ni mojawapo wa sifa muhimu katika uhakiki wa msuko.Msuko huu una mvuto kwa msomaji kwa sababu Susan aliye mmoja wa wahusika wakuu anawakilisha msimamo wa watu wengi ambao wangependelea wazazi wawapatie watoto wao fursa ya kutangamana na wenzao.

### 2.3 Visuko

Kisuko cha kwanza ni kati ya Richard na mkewe Mary Kasiva. Mary ni mama wa nyumbani. Yaani hakuwa na kazi maalum. Alimwogopa sana mumewe. Aidha alimwachia mumewe kazi ya malezi. Watoto wake walipoenda kucheza na watoto wa jirani jambo walilokatazwa, Mary Kasiva aliwashtua kwa kuwaambia atawashtaki kwa baba yao. Tunashangaa kwa nini yeye hangewadhibu kama mzazi. Mary anawakumbusha kuwa baba yao ashakataza jambo lile.

Yeye hakuhusika sana na mafundisho ya Biblia lakini alibaki kufuata mapenzi ya bwanake. Alipoulizwa na mwanawe sababu za kukubaliwa kucheza na watoto wa jirani, hakuwa na sababu nzuri. Watoto wa familia hii walielewa mama yao hakuwa na usemi mbele ya baba yao. Mary hangeweza kumkataza bwanaye kuwachapa watoto wake. Msimamo wa Richard wa kidini ulijulikana na wazee na akina mama wa kijiji chake.

Wanawake wachache walimwonea Mary gere kwa kudhania kaishi maisha mazuri. Waliona alikuwa na bahati nzuri kwa kuishi na mtu wa Mungu. Wengine walimsengenya. Labda walishangaa jinsi alivyoweza kuishi na mume mwenye misimamo mikali ya kidini. Mary Kasiva aliheshimu utamaduni. Alimsisitizia mumewe ilivyokuwa vibaya kukata mkuyu kama alivyokanywa na mzee fulani.

Tunafahamishwa kuwa Richard alipokataa kutii, mkewe alibaki kumwangalia tu. Mary Kasiva aliishi kwa hofu kuu, aliogopa mumewe kiasi kwamba hakuwakosoa watoto wake walipokosea. Hakuonekana akisumbuka kwa makosa ya watoto wake. Tunamwona wakati mmoja Susan alipoandamana na wenzake kwa bahati mbaya akachelewa mamake alimwambia kuwa kitendo hicho ni cha kumzulia matata ya bure. Anashangaa atakachomweleza mumewe hili linaonyesha kuwa hakuwa na uhuru katika maisha yake na hasa mbele ya mmewe. Wakati wowote alipoongea mbele ya mmewe alitupiwa mkodoo wa macho.

Mary aliona mzigo mkubwa wakati watoto wake wangekosea. Swali kubwa lilikuwa mume wake angesemaje? Tunamwoa wakati Roselyn alipomaliza mtihani wa darasa la nane na kuchelewa kurudi nyumbani, alisumbuka sana mawazoni. Yawezekana uwoga huu ulitokana na pigo alilopata mwezi wa pili baada ya kujifungua mtoto wa kwanza. Mary alijuta kutokuwa na uwezo wa kumtetea mwanawe wakati ambapo alikuwa akipigwa na baba yake.

Tunamwona Mary wakati fulani baada ya Roselyn kupokea kichapo kikali na kuachiliwa, Mary alimfuata nje kwa huruma ishara ya kuwa, udhaifu aliokuwa nao ulimzuia kumkinga mwanawe. Tukio lingine linaloonyesha udhaifu ni wakati Susan alipomkosoa babake baada ya Roselyn kufukuzwa. Anashangazwa na ukakamavu wa Susan.

Kisuko kingine tunakipata kati ya Susan na mwalimu Octavian Birundu. Birundu alikuwa mwalimu wa sayansi. Aidha alikuwa mkuu wa kundi la uigizaji shuleni. Birundu alimshawishi Susan kujiunga na kundi hili la uwigizaji. Wakati huu Susan alikuwa mwanafunzi wa kidato cha tatu. Tunaelezwa siku moja mwalimu Birundu alimtuma mwanafunzi mmoja kumwita Susan.

Jambo hili halikumfurahisha Susan kwa sababu tunampata akiwaza kuwa badala ya kumpelekea shida zake angechagua kumwachia Mungu. Nyumba ya mwalimu huyu ilikuwa mahali pembani na sheria za shule hasikuwaruhusu wanafunzi kutembea kwa walimu.

Siku moja mwalimu mkuu hakuwa shuleni, kwa hivyo Susan aliamua kutembea kwa Birundu ili kujua alichomwitia hata ingawa alikuwa na woga. Mandhari ya nyumba yake haikupendeza sana. Susan alipofika na kubisha alikaribishwa na kuingia lakini kwa wasiwasi mwingi sana. Mwanzoni alichelea kuketi lakini hatimaye aliketi.

Mtunzi hatwaambii mengi baada ya Susan kuketi ila tu mazungumzo mafupi kati yake na Bethsheba juu yao kujiunga na kundi la kuigiza. Wakati huu Birundu alikuwa chumba cha ndani.Hatuambiwi alichokuwa akifanya mle ndani.

Kisuko kingine kinazunguka Richard akiwa shuleni. Richard alisomea shule moja ya upili iliyoitwa Skyway. Ilikuwa shule ya kibinafsi. Richard Ngunze hakulala shuleni hata ingawa shule yenyewe ilikuwa ya bweni. Alipanga chumba kwenye duka moja mtaani Swahili. Alipofika kidato cha nne hali yake ya afya ilianza kuharibika. Kichwa chake kilianza kumuuma na pia kuumwa na viungo vya mwili kama vile kutatizwa na miguu yake pamoja na viungo vingine. Hali hii ilimfanya aachane na masomo yake. Shida hii aliipeleka hospitali lakini hakupata msaada wa kudumu. Mamake hakunyamaza bali alitafuta msaada kutoka kwa wengine.

Alipopata ushauri kuwa kulikuwako na mganga fulani maarufu, basi siku moja alirauka asubuhi na mapema kuelekea kwake. Baada ya kufika nyumbani kwa mganga Syokulu alifanyiwa sarakasi za uchawi.

Matokeo ya sarakasi hizi yalikuwa, mwanawe alikuwa amerogwa na mamake wa kambo yaani mamake Stephanus kwa madai kuwa alimwua binti yake. Basi Nzisa aliamuliwa ampeleke mtoto wake pamoja na jogoo, kipora na kinyesi cha ngawa.

Richard alitibiwa na kurudi shuleni. Baada ya kurudi shuleni, babake alipata ugonjwa. Alitafutiwa matibabu kutoka kwa wachawi mbalimbali akiwapo Syokulu lakini hakuna aliyepata tiba yake. Nzimba wa Mutembei alikata roho baada ya muda mfupi. Habari ya kifo cha baba yake Richard ilimfikia alipokuwa shuleni na ilikuwa wakati wa mtihani wa kidato cha nne. Wakati huu alikuwa bado na maumivu ya mwili. Maumivu ya kichwa ndiyo yalimtatiza sana.

Mtunzi anaendelea kutwambia kuwa baada ya Richard kufanya mtihani na matokeo kutangazwa, hakuwa amefanya vizuri kama alivyotarajia. Jambo hili liliwashangaza hata walimu wake. Hali hii haikumruhusu kuendelea na masomo. Hali ya maisha kwake haikuwa rahisi tena. Alianza maisha ya kujitafutia riziki. Kibera Laini saba ni sehemu aliyojaribu bahati yake.

Tunaelezwa kuwa haikuwa rahisi kupata kazi lakini alipata vibarua katika maeneo mbalimbali kama vile kampuni ya kuuza mafuta, kampuni ya watengenezaji wa pombe ya Breweries, Yakuza Tourists Firm kati ya kwingineko. Alipokuwa katika Yakuza Tourists kama tarishi, alianza urafiki na msichana mmoja jina lake Agnes Mbula. Richard alimwona Mbula akiwa mrembo aliyeumbwa vizuri. Agnes alifanya kazi ya kuuza duka ya urembo. Urafiki wao ulianza kimchezomchezo na kupea na kuwa mapenzi. Muda usiokuwa mrefu baada ya Richard kurudi kazini kutoka likizoni Mbula alimweleza kuwa urafiki wao haungeendelea.

Baada ya kuachwa na mpenzi, Richard alipatwa na pigo la kufutwa kazi. Siku moja Richard akiwa Uhuru Park alikuta mahubiri yakiendelea. Baada ya kusikiliza kwa muda, alivutiwa na kilichokuwa kikiendelea na kukata shauri ya kumkubali Mungu.

Richard baada ya kusikiliza kwa muda aliamua kurudi nyumbani ambako asingekosa jambo la kufanya. Hili lilifanyika baada ya kukaa bila kazi kule mjini. Tunaelezwa kuwa Richard alipokuwa safarini na baada ya kufika Machakos mahali alitua kwenye duka fulani kupata soda.

Hapo alikutana na msichana aliyemwona mara ya kwanza Uhuru Park. Baada ya mazumgumzo marefu urafiki ulijengeka na mbegu ya mapenzi ikapandwa.Jina la msichana huyu lilikuwa Mary Kasiva. Msichana huyu ndiye baadaye alikuja kuwa mke wake Richard Ngunze.

Riwaya hii ina kijiploti kingine kinachowazunguka Mary Kasiva na mwajiri wake Deogratias Manyara. Kasiva alipoacha shule katika shule ya wasichana ya Mbooni kwenye kidato cha pili, alijiunga na shangazi yake mjini Nairobi. Hii ni baada ya wazazi wake kushindwa kugaramia masomo yake. Kusudi la kujiunga na shangaziwe ilikuwa ili apate kazi. Baada ya muda fulani kupita alibahatika kupata kazi ya uyaya mtaa wa Kileleshwa uliokuwa mtaa wa matajiri. Mwajiri wake alikuwa mkurugenzi wa *MG Contractors*.

Mkewe Manyara alikuwa mfanyi biashara kwenye maduka ya kuuzia urembo: vipodozi, mafrisho na kila aina ya mafuta. Bi Manyara alizoea kusafiri nchi za nje katika shughuli za kibiashara. Kasiva alipata mshahara mkubwa na alimsaidia kitinda mimba wao kwa kumlipia karo ya sekondari. Wazazi wake walifurahia jambo hili sana.

Manyara alianza tabia ya kurudi nyumbani. Mara kasema kasahau na jalada la kazini mara nyingine ingekuwa kitabu cha hundi za benki au funguo maalum. Mara angemletea Mary zawadi.

Mary na Manyara hatimaye wakawa wapenzi. Hatima ya mapenzi haya yalimpelekea Mary kuwa mjamzito. Mary aliiavya mimba hii na akawa sasa na hadhari. Bila kuona hatari nyingine tabia ile ile ilianza tena. Haukupita muda mrefu kabla Bi Manyara kuwafumania.

Tukio hili lilimfanya Mary kufutwa kazi akiwa na mimba ya Manyara. Shangazi yake hangemruhusu Mary kuavya mimba hii kwa msingi kuwa alikuwa mkristo. Ni wakati huu aliandamana na shangaziye kwenye mkutano wa mahubiri Uhuru Park Richard Ngunze alipomwona mara ya kwanza. Walipokutana na Richard Machakos, walikumbukana na kukumbushana mkutano huu.

Kisuko cha mwisho kinawahusu Mary Kasiva na Richard Ngunze kwenye miezi michache baada ya harusi yao. Ilikuwa mwezi wa saba baada ya ndoa yao kufungwa. Mary alianza kulalamika kuwa anasumbuliwa na maumivu ya tumbo. Hali hii ilimtia hofu Richard asijue kana kwamba yalikuwa maumivu ya kujifungua. Alijituliza kwani ulikuwa mwezi wa saba baada ya kuoana. Alianza kuwa na wasiwasi kama hiyo mimba ilikuwa yake au haikuwa yake. Maumivu yalipozidi iliamuliwa Mary apelekwe hospitali. Walipofika, mojakwa moja Mary alipelekwa chumba cha kujifungua.

Richard alikuwa asubiri nje kwa muda. Akiwa pale nje Richard alikuwa na wasiwasi mwingi kwa tukio kama hili asilokuwa ametarajia. Baada ya muda Mary alijifungua mtoto na alipomtazama alichukua sura ya Manyara aliyekuwa mwajiri wake hapo awali. Richard alitamani sana kupata habari ya yaliyokuwa yakiendelea mle ndani na ikiwezekana kuingia kumwona mtoto wake. Alitarajia mtoto awe wa kiume. Hatimaye Richard alikaribishwa ndani na nesi. Alimtupia mtoto macho, hakuona sura yake mwenyewe wala ya bibiye. Kwa mara ya kwanza akamshuku bibiye.

Nesi hawakuelewa kilichokuwa kinaendelea akilini mwa Richard kwani alitawaliwa na ukimya usiokuwa wa kawaida. Hali yenyewe ilimfanya Richard kumeza mafunda ya mate machungu. Hali hii haikumfaa wala kumfurahisha. Alishindwa kumsamehe mkewe.

Riwaya ya *Nguvu ya Sala* ni changamano. Riwaya yenye ploti zaidi ya moja. Muundo wa aina hii huhitaji basi msomaji aisome riwaya hii kwa makini ili aielewe vyema ili kuridhisha lengo lake. Ploti zake tumezishughulikia kama tulivyotaja hapo awali.

Riwaya ya Nguvu ya Sala ina mvuto kwa wasomaji, ina wahusika ambao wanatuvutia sisi wasomaji na tungependa kusimama nao. Katika msuko kuu ya Susan na baba yake inatuvutia sana kwa sababu tunawaona wahusika hawa wakivuta kila mmoja upande wake.

Susan anataka uhuru naye baba yake anataka malezi mema kwa watoto wake. Tunampenda Susan kwa juhudi alizonazo kutetea uhuru kwao nyumbani. Mambo yalipoharibika nyumbani kwao baada ya Roselyn mnuna wake kufukuzwa kwa kupata mimba, Susan alimkosoa babake ambaye alikuwa mkali. Katika dondoo hili tunaelezwa yafuatayo,

> Nadhani mmekosea… kumfukuza Roselyn hakukusuluhisha lolote wala sio njia ya kuwaondoea aibu… Haya ni mawazo mabayababa. Isitoshe, watoto wote ni sawa. Jamii yetu imekuwa ikimdharau mwanamke kwa sababu ya kutojua. Imebaki mtumwa wa mawazo ya kizamani. (uk 195, 197).

Kutokana na dondoo hili, tunamwona Susan akijibizana na babake jambo ambalo hakuna aliyelifanya hapo awali. Mamake Susan alipata mwanawe akiwa na ukakamavu wa hali ya juu jambo aliloliona kana kwamba lingemletea balaa baadaye.

Mary mama yake Susan anamshawishi kuachana na mambo hayo. Anasema "Achana na maneno hayo Susan," (uk 198). Baada ya pambano hili, Richard aliona ukweli wa mambo na kutumana Roselyn atafutwe na arudi nyumbani. Tunasoma hivi,

> Mwache bintiyo aongee atakavyo, alisema baba mwenyewe kalegea kama mgonjwa wa kifafa. Aliyatuliza macho yake ukutani kwa muda mrefu nilihisi kuwa alikuwa akiyacheua maneno yangu. Baada ya kipindi kirefu alisema.Kesho nenda kwa Nicodemus ukamwambie dadako arudi nyumbani. (uk. 198).

Hapa tunapata kuwa baba amebadili msimamo. Kama wasomaji tunampa Susan heko. Mgogoro baina ya Susan na baba yake unaukuza msuko huu kwa njia inayompata msomaji ilhamu ya kuendelea kuisoma riwaya. Wakati Richard alipompelekea mkewe hospitali kujifungua tunamwona akiwa na mgogoro wa kimawazo. Tunaelezwa,

> Mawazo ya kila aina yalianza kukimbizana katika akili yake. Mm…inawezekana akawa na maumivu ya kujifungua? Lakini huu mwezi ni wa saba tu inawezekana mtu akajifungua hata baada ya miezi saba.Ni vigumu. Si ajabu. Hasa kwa mtu anayejifungua kwa mara ya kwanza. Mm... sidhani. Labda hiyo mimba si yangu! Haiwezekani! (uk 179, 180).

Hapa tuaona kuwa Richard amechanganyikiwa asijue ukweli wa mambo. Mgogoro mwingine unapatikana wakati Susan alipokuwa akimkosoa babake kama vile tumejadili hapo awali. Susan anaeleza: “Nadhani mmekosea…….” (uk 195).

Huu ni wakati Susan alimshambulia babake kwa sababu ya kumfukuza mnunawe. Katika msuko unaowazunguka Susan na mwalimu Octavian wakiwa kwake nyumbani baada ya kumwalika.

Tukio hili linatuacha tukijiulliza, je mwalimu Octavian alimwitia Susan nini kwake nyumbani? Sehemu hii inakuza taharuki kwa msomaji ambao wanaishia kuwa na maswali mengi. Tunapata taharuki nyingine kwenye ndoto ya Richard alipokuwa mgonjwa wakati wa mtihani wa kidato cha nne.

Kwenye ndoto aliota akikimbizwa na mnyama aliyekuwa na mapande mawili ya ulimi yaliyoandikwa MORTIS na upande wa pili ANGST. Ndoto hii inaishia mahali ambapo pande moja la ANGST lilikuwa karibu kumpata (uk 55, 56).

Tunaachwa kujiuliza kama lilimpata au la? Na kama lilimpata lilimfanya nini? Aidha, tunapata sifa ya mshangao wakati mkurugenzi wa kampuni Bwana Manyara alipofumaniwa na mkewe kwenye kitendo cha mapenzi na yaya wake wa nyumbani. (uk. 165, 167).Hatungetarajia haya yafanyike kwa mtu aliyeheshimika kama yeye. Aidha, tunashangaa kwani hakuacha tabia hiyo yaya wake alipopata mimba mara ya kwanza na kuiavya. Sifa ya mbinu rejeshi inajitokeza katika riwaya hii. Riwaya yenyewe inaaza kwa familia nzima ya Richard. Yaani tunamkuta Richard, mkewe na hata watoto. Lakini baadaye kidogo tunaletewa maisha ya Richard akiwa shuleni, akitafuta vibarua na hatimaye akifunga ndoa.

Aidha, tunayapata maisha ya mkewe akiwa shuleni, akiwa yaya nyumbani mwa Manyara na hatimaye akifunga ndoa. Mbinu hii hutumika ili kufafanulia msomaji mambo zaidi. Mtunzi wa kazi hii amefaulu katika kueleza misuko yake.

## 2.6 Hitimisho

Katika sura hii, tumeangalia msuko na visuko mbalimbali. Misuko imekamilishana kuunda kazi nzima. Tumepata kuwa, kuna msuko mkuu na visuko vingine vidogo.

Visuko hivi vimechangia kuunda msuko mkuu.  Imebainika kuwa ingawaje kila msuko unalenga swala tofauti. Maswala haya yana uhusiano na maudhui makuu ya kazi hii ambayo ni malezi na dini.

# SURA YA TATU

# MANDHARI KATIKA NGUVU YA SALA

## 3.1 Utangulizi

Mandhari ni kipengele mojawapo muhimu sana katika fasihi kuingana na Wamitila (2001), mandhari hutufichulia ni wapi na lini ambapo matukio fulani yalifanyika. Mandhari hutumiwa kurejelea wakati na sehemu ambapo matukio ya msuko hutokea. Kimsingi mandhari hutumiwa kurejelea mahali panapotendeka tendo fulani. Mandhari fulani inaweza kuathiri tabia na lugha ya wahusika. Kazi yetu itachunguza mandhari ya mjini, mandhari ya mashambani hatimaye mandhari ya shuleni. Kwenye sehemu hii tutachunguza jinsi ambavyo mandhari yanavyowaathiri wahusika.

## 3.2 Mandhari ya Mjini

Msanii anatuchorea mandhari ya mji wa Machakos. Mji huu ndimo shule Richard Ngunze aliyosomea. Msanii anatwambia kuwa shule hii ilikuwa kwenye kiini cha mji wenyewe. Sehemu hii ya mji mahali shule ilikuwa, ilikuwa na shughuli za kila aina. Watu walipenda sehemu hii na wengine waliuchukia. Kulikuwa na msikiti mkubwa. Tunafahamishwa juu ya mtaa wa Swahili ambao ulikuwa upande wa mashariki. Mabanda yaliyokuwa pale yalikuwa mabovu ambayo msanii anayafananisha na mbavu za mbwa.

Mji huu haukukosa umati wa watu usiku na mchana. Watu waliokuwa mle mjini walikuwa wa sampuli mbalimbali yaani watoto, watu wa makamu na wazee. Hali ya maisha ilikuwa ya chini.

Hili tufahamishwa na jinsi watoto walivyokaa uchi kwa kukosa mavazi. Mara kwa mara wanawake walionekana wakitoka mabandani wakijifunga leso kama kwamba ndio wanaamka.

Upande mwingine wa shule kulikuwa na bwalo la maofisa. Wakati wa saa saba watu walijaa eneo lile. Msanii anatundokezea ya kwamba Richard hakukaa katika bweni la shule bali alipanga chumba kidogo kwenye duka moja lililokuwa katika mtaa huu uliojaaa kila aina ya anasa na shughuli nyinginezo. Chumbani hakuna mpangilio wa vyombo. Tunaambiwa ya kuwa vyombo hivyo vilisukumizwa kwenye kiini cha mvungu wa kitanda. Nguo ziliangikwa ukutani na nyingine zilininginia juu ya kamba iliyofungwa juu ya kitanda.

Mandhari ya namna hii sio salama hata kidogo kwa mwanafunzi. Hata ingawa mhusika huyu hapatikani akijingiza katika anasa zinazoendelea Katika mtaa wa Swahili anu mji wote kwa jumla, kelele na kila aina ya shughuli kweli yangetatiza juhudi zake za kumakinika katika masomo yake. Hivyo mandhari haya yalimwathiri vibaya Richard Ngunze.

Mandhari mengine ya mjini yanapatikana mjini Nairobi kwenye mtaa wa Kibera Laini Saba. Tunampata Richard Ngunze akiishi hapa kwenye chumba kimoja na rafikiye. Mtaa huu ulikuwa wenye nyumba za mabanda ambayo yalikuwa yamejinamia kama mbavu za mbwa. Yaani yalikuwa mabaya. Chumba hiki kilikuwa katibu na kijito kwenye maji machafu yalikuwa na harufu mbaya. Harufu hii ilimtatiza Richard sana hasa siku za mwanzo mwanzo. Kwenda kwake mjini alienda kwa lengo la kutafuta kazi. Haikuwa rahisi kupata kazi. Siyo kwake tubali hata na kwa wengine. Mwandishi anatueleza kuwa mhusika huyu hakupata mlo kwa siku kadhaa. Wakati fulani twaambiwa alipata kichomi kilichosababishwa na kukosa kula kwa muda.

Siku moja wakati alikuwa amejilaza kitandani akipumzika alisikia katika chumba cha jirani mwanamke mmoja na mwanaume wakipigia bei bidhaa fulani.

Baada ya kuelewana wale watu walitulia na Richard akasikia kuhemahema kisha mpumuo na mwishowe kicheko jambo tunaloweza kudhaniwa wahusika walikuwa kwenye kitenda cha mapenzi. Mandhari haya hayakuwa salama kwa sababu yangensawishi Richard kuingilia anasa ambayo ingeathari zake. Kama vile magonjwa ya zinaa upachikaji wa mimba na mambo kama hayo.

Mandhari ya mwisho tutakayoangalia yanapatikana mjini Nairobi sehemu ya Uhuru Park. Mhusika tunayemkuta hapa ni Richard. Mandhari haya yalikuwa na watu wengi sana siku hii. Palikuwa na mkutano mkubwa wa kidini jambo liliwafanya watu kujumika vile. Hali ya anga ilikuwa shwari hivyo alifikiria kujiunga nao. Wahubiri walikuwa mzungu na mwafrika. Mhubiri alikuwa mzungu na mwafrika mkalimani. Msanii anatwambia baada ya muda mrefu Richard alianza kuvutiwa na maneno ya jamaa hawa na kusawishika polepole. Alianza kusikia uwazi fulani ndani yake. Matamko kama vile ulimwengu umejaa uchafu, watu wamegeuka makatili, uzinzi umeongezeka , uhuni na ukahaba amani hamna na mambo kama haya.

Baada ya haya wale wahubiri walifanya mwito. Richard alikata kauli na akamua kumkubali Bwana kwa kuinua mkono wake ishara ya kukubaliana na yaliyokuwa ya kiendelea. Mandhari haya pamoja na yaliyokuwa yakiendelea yaliathiri maisha yake na kuwa mfuasi wa dini maisha ya Richard ya baadaye tunayapata akiwa kiongozi wa kanisa na kuhimiza mafundisho ya Biblia katika familia yake.

### 3.3 Mandhari ya Mashambani.

Mandhari ya mashambani tunayakuta kwa Richard Ngunze. Hapa tunamkuta akiwa sasa ana familia ya mke na watoto. Hii ni baada ya kuchoshwa na maisha ya mjini na pia baada ya kupeana maisha yake kwa Mungu.

Kwenye mandhari haya Richard anaingoza familia yake kwa mafunzo ya Biblia na anamini nguvu zinazotokana na sala yaani maombi. Majirani walifikiria kuwa familia yake ilikuwa na bahati kwa sababu ya msimamo huu. Katika mandhari haya hakukuwa na kazi maalumu mhusika huyu aliyofanya bali alifanya kazi ya kulima na mwisho wa Juma kuhudumia wafuasi wa kanisa alilokuwa akiliongoza. Maisha katika nyumba ya Richard hayakuwa rahisi hasa kwa watoto wake.

Watoto walikatazwa kucheza na watoto wa jirani eti hawakuwa Wakristo. Hali hii haikuwafurahisha kwa sababu wanauliza mama yao kwani ubaya uko wapi (uk 2). Mama anapojibu anasema kuwa baba yao alikataza haya. Mama watoto anasema kuwa atawasema kwa baba yao akirudi. Hapa kama wasomaji tunajiuliza kwa nini asingewadhibu yeye mwenyewe, badala ya kungojea baba yao. Hili linatufanya kufikiria kuwa mama watoto hakuwa na uwezo mkubwa kutawala familia yake kama mzazi. Ni kama kwamba alimwogopa mumewe kiasi kwamba hakuwa na haki ya kuchukua hatua dhidi ya watoto wake.

Katika mandhari haya tunaelewa kuwa Richard ametawaliwa na mawazo ya kitamanduni kuwa mwanamke hana usemi mkubwa hasa mbele ya mwanamume. Sababu inayofanya tuseme haya ni kuwa kwenye (uk 196), Richard anasema kuwa hawezi kukosewa heshima na mtoto wa kike. Anakosolewa mawazo hayo na Susan mtoto wake anapoambiwa kuna watoto wote ni sawa.

Aidha sababu nyingine inayotuonyesha kuwa Richard ametawaliwa na utamaduni wa kudunisha mwanamke ni wakati Richard anasema kuwa yeye hajawahi kustahili mabishano na wanawake (uk 197). Mafundisho ambayo Susan aliyapata nyumbani yalimwathiri kiasi kwamba aliweza kijiepusha na mienendo mibaya ya rika yake pale shuleni.

Susan alipopelekwa katika shule ya upili mara yake ya kwanza waliwakuta wanafunzi wakiongea huku wakiangua vicheko. Susan aliona jambo hili likiwa mbaya sana. Hii ilikuwa kwa sababu ya mafundisho aliyoyapata kutoka kwa baba yake kuwa hii haikuwa tabia nzuri. Susan anatueleza yafuatayo;

> Baba alichukia tabia hii ya kuangua kicheko. Alisema kuwa haikuwa tabia nzuri kwa watoto wa kike. Nakumbuka jinsi alivyonicharaza siku moja baada ya kunisikia nikicheka kwa sauti ya juu. Niliamini tabia hii ilikuwa mbaya na haikosi Mungu aliichukia. ( uk 33).

Tunapata kuwa Susan aliweza kuamua hali ya mambo kutokana na jinsi alivyofunzwa hapo awali. Athari ya aina hii ni nzuri kwa kuwa tunamwona Susan akizingatia staha katika maisha yake. Pia tunapata tukio lingine linalotupa athari ya mafundisho ya mandhari ya mashambani yaani nyumbani mwa Susan. Susan akiwa shuleni karibu na uwanja, alishangaa vipi mwenzake Fortunata aliweza kuwa na rafiki wa kiume ingawaje alikuwa darasa la nane. Jambo hili hakuliona likiwa nzuri kama alivyofunzwa. Susan anasema hivi,

> Sikuweza kushangaa jinsi ilivyowezekana kuwa Furtunata kuwa na rafiki wa kiume alipokuwa darasa la nane. Nayakumbuka maneno ya mama kuhusu wavulana.

> Alinishauri niwapuuze na sio kujipuuza nao tu bali kujibari nao. Wavulana ni laghai na hawaaminiki. Ukifanya kosa la kukaribiana nao utajuta kuzaliwa hivyo ndivyo alivyonishauri mama. ( uk 44).

Susan anatueleza kuwa mashauri haya aliyaamini. Ilifaa Susan kuyazinagatia mashauri kama haya kwa sababu kweli yangemfaidi katika siku za baadaye. Mwandishi anaendelea kutuletea matukio zaidi yanayotusaidia kuona jinsi Susan alivyoathiriwa na mafunzo ya mandhari ya nyumbani. Tunaambiwa kuwa Susan akiwa shuleni alikumbwa na shida ya maumivu. Maumivu haya hakuwa ameyapata hapo awali kwa hivyo yalimshtua kiasi. Hata hivyo aliweza kujimudu vilivyo kutokana na kumbukumbu ya mambo aliyofunzwa nyumbani. Baadhi ya mambo haya ni kama anavyotueleza hapa kutoka kwa wazazi wake,

> Jitunze vizuri mwanngu ili usiniaibishe mimi! Alisema baba. Mm! mwanangu usimwaibishe babako, alisisitiza mama. Kumbuka utapatana na majaribu ya kila aina mwanangu, alisema baba. Kumbuka uwezo wa maombi, alisema mama…usisahau nguvu ya sala. (uk 60).

Dondoo hili ni kumbukumbu ya Susan akiwa shuleni baada ya kupata shida. Kweli Susan alikubaliana na ushauri huu kwa sababu baada ya kukumbuka haya aliingia katika maombi ikiwa njia ya kutatua shida yake aliomba ifuatavyo,

> Bwana naomba unieleze ipasavyo. Naomba usinitie katika vishawishi. Nipe nguvu za kuweza kubadili na kuzishinda hila za mwovu. Nielekeze jinsi ya kulitunza kanisa lako bwana. Kwa jina la Kristo naomba ( uk 61).

Susan akiwa katika hali ya kufikira kilichosababisha maumivu yale; Sista Emily ambaye alikuwa nesi wa shule alimkuta katika hali ya kufikiria sana juu ya shida yake. Kama mtu aiyekuwa na huruma na pia likiwa jukumu lake kama nesi alimuliza Susan alichokiwazia namna ile. Tunaelezwa kuwa Susan hakuweza kujibu kwa haraka. Tunaambiwa kuwa Susan alijaribu kukwepa kujibu maswali aliyoulizwa. Sehemu hii pia ni muhimu kwetu kwa sababu hata ingawa Susan aliongea uongo alijua dhahiri kuwa lilikuwa jambo baya na akakiri kuwa alijua lilikuwa mbaya. Basi tunaelewa kuwa alipata alivyofunzwa na baba yake. Susan anaeleza hivi,

> Nilishindwa kumjibu kwa haraka ilinibidi kumlazia. Nawazia maneno yako hayo nilisema. Nilijua kuwa ulikuwa uongo. Baba aliuchukia uongo, alishikilia kusema kuwa huo ulikuwa upotovu wa kishetani. (uk 63).

Wanafunzi waliosoma na Susan mara kwa mara walishangaa kwa nini Susan hakumwendea mwalimu aliyetwikwa na jukumu la kuwashauri wanafunzi walipopatwa na shida mbalimbali. Susan alipokuwa anawajibu aliwaambia kuwa mambo yaliyomshinda alimwachia Mungu. Tunaelezwa haya na mhusika huyu,

> Mwanafunzi mmoja wa kidato cha kwanza alinijia na kuniarifu kuwa niliakiwa na mwalimu wa sayansi, Octavian Birundu. Huyu ndiye aliyekuwa mshauri wa wanafunzi katika shule yetu na tulipaswa kumwendea kila tulipokuwa na tatizo lolote. Mambo yaliyonishinda nilimwachia Mungu. Nilimwasilishia udhia na kero zangu. Nilimwachia dhiki na masumbuko yangu.

> Nilimtegemea kwa kila kitu kwa kuyakumbuka maneno ya baba kuhusu nguvu ya sala. (uk 67).

Susan alielewa kuwa katika shida na mahitaji yake katika maisha, Mungu wake alikuwa na uwezo kupitia nguvu ya sala. Kupitia kwa athari hii aliweza kuendeleza maisha yake vizuri. Hakuishi kama mtu ambaye hakuwa na matumaini katika maisha. Mwandishi anaendelea kutupa matukio zaidi ambayo yanatupatia mwangaza kuhusu kufaulu katika mambo mengi kwenye maisha ya Susan kutokana na athari za maisha yake akiwa kule mashambani. Kwenye tukio jingine wachezaji wa mchezo wa kuigiza wa shule yake yeye akiwa mmoja wao walikuwa katika shule ya wavulana ya Machakos.

Susan alihitajika kumzindikisha mwanafunzi mwenzake dukani ili kununua vitu fulani. Tunaelezwa kulikuwa usiku na giza lilitawala. Tunaambiwa kuwa giza lile lilimtia wayo wayo na pale pale akakumbuka maneno ya baba yake, "Shetani hupenda giza mwanangu tahadhari sana na giza…m… mwanangu tahadhari sana na giza. Tembea katika nuru tu. Je, giza alilozungumzia ni giza la aina hili? Niliemewa natamani kurudi." (uk 76).

Kumbukumbu ya mambo haya hayamwachi bure bali anajihoji na kufanya matengenezo yanayohitajika. Mafundisho ya nyumbani yanayoonekana yenye athari kubwa katika maisha yake na yanamsaidia kwa kiwango kikubwa sana. Baada ya mchezo wa kuigiza kuisha, tunawakuta Susan na mwalimu Birundu wakitembea pamoja. Mwalimu huyu alionekana akitembeatembea karibu na Susan jambo ambalo lilimshangaza Susan. Baadaye kidogo mwalimu Birundu aliutupa mkono wa kulia na kuushika mkono wa Susan wa kushoto.

Susan alishtuka ghafla na kuuvuta mkono wake kwa nguvu. Tunaambiwa Susan alitamani kumkemea lakini hakuweza. Maneno yalimkwama kooni na ulimi ukamvimbia kinywani.

Majibizano yaliyofuata baadaye yaonyesha wazi kuwa Susan hakuwa tayari kwa yale Birundi alikuwa nayo mawazoni. Susan alidai kuwa hata babake hamshiki alivyofanya Birundu.

Haya yote yanaonyesha kuwa alipata vizuri ushauri wa wazazi wake kuwa alifaa kwa vyovyote vile kujitenga na wanaume ilivyowezekana. Tunabaki kumpa Susan heko kwa sababu akiwa mbali na nyumbani hakuacha mashauri ya wazazi wake. Susan anatueleza hivi,

> Alitupa mkono wa kulia na kuushika mkono wangu wa kushoto. Nilishtuka ghafla na kuuvuta mkono wangu kwa nguvu. Nilimwangalia mwalimu Octavian aliyekuwa akichekacheka tu. Nilitamani kumkemea lakini sikuweza. Maneno yalinikwama kooni na ulimi ukanivimbia kinywani. Ghadhabu ilinitishia kuniziba pumzi. Mm… Susie hu mtoto tena. Ni nini unachoogopa? Aliuliza mwalimu. Mbona unashika mkono wangu? Niliuliza kwa hasira. Mm Susan kwani kushikwa mkono kuna nini? Hivi babako hakushiki mkono aliuza. (uk 79).

Haya yanatundokezea madili mema tunayopata katika maisha ya Susan. Anaibuka kuwa kielezo chema. Susan akiwa shuleni tunamkuta akikumbuka jinsi alivyoelezwa na mama yake kuwa njia pekee ya kumfurahisha ni kwa kupita mtihani wa kidato cha nne na kufuzu kujiunga na chuo kikuu. (uk 90). Susan alijikaza kuelewa na vipengele muhimu kama vile *Binomial theorem… Pythagoras theorem* ili aweze kupita mtihani wake.

Hapa tunaona wazi kuwa mashauri haya aliyoyapata katika mandhari ya nyumbani yalimwathiri vyema na kumfanya kutia bidii masomoni pindi alipoyakumbuka. Hivyo kuinua hali yake ya masomo.

Mandhari ya mshambani ambamo alipata mafundisho ya Biblia pia yalimpa maadili mema ambayo yalimsaidia kuwa mtu mwaminifu asiyependa kushiriki maovu.

Tukio linalotundokezea haya ni wakati Susan alikuwa kwenye maktaba kule shuleni. Tunampata Rose rafiki yake akija na karatasi la mtihani ambalo alipewa na mwalimu Octavian kwa njia ambayo haikuwa halali. Haikuwa njia halali kwa sababu mtihani huu ulikuwa bado haujafanywa na ulikuwa ufanywe baadaye. Tunamwona Susan alipodhibitisha kuwa kwa hakika ulikuwa mtihani alipigwa na butwaa kwa kushangaa kuwa uovu ule ungefanyika. Susan anamuuliza Rose, “Huo si ni wizi Rose?” (uk 94).

Susan anaonya kuwa sheria za Mungu zinakataa wizi wa aina yoyote. Katika mazungumzo yao na Rose aliyekuwa ameshiriki wizi ule anachangia kuwa, watu walikwisha vunja sheria za Mungu zamani. Hivyo kubabaika Susan alikoonyesha hakukuwa na msingi wowote. Bila shaka mafundisho Susan aliyoyapata akiwa nyumbani yalimsaidia pakubwa. Tunafurahishwa na msimamo wa mhusika huyu. Katika akili ya Susan kulikuwa na mvutano mkubwa sana juu ya karatasi lile la maswali. Tunamuona akidai kupewa maswali yale ayaone lakini dhamiri yake ilikuwa ikimkataza kwa hali ya juu. Sehemu moja ya akili yake ilimhsauri asidanganye. Sehemu nyingine ilimwambia huku hakukuwa kudanganya, Susan anatueleza hivi,

> Huu ndio mtihani! Kumbuka kudanganya ni hatia mbele ya Mungu. Wala siye mimi miliyekwenda kuichukua karatasi yenyewe. Haijalishi kama hukwenda ichukua mradi umeyaona maswali tu. Anayekamatwa na ngozi ndiye mwizi. Hamna shida, nitaomba toba Jumapili.

> Hiyo tabia si nzuri kumbuka alivyosema babako. Mm… kudanganya huwa hatua ya kwanza katika uasi. Hayupo hapa baba. Lakini Mungu anayaona haya.
>
> Usipende kushiriki katika uhalifu. Haijalishi kama unaasi sheria za Mungu au la. Hili ni suala la udanganyifu. (uk 96).

Mvutano huu katika akili ya Susan uliishia kwake kuamua kuwa haikuwa vyema kuiba ule mtihani kwa sababu aliona Mungu alikuwa anamuona akitenda kitendo kile. Hivyo athari ya mafundisho ya nyumbani yalitawala katika akili yake na kujiepusha kabisa na tendo lile ovu lililomkabili mhusika huyu. Mashauri aliyoyapata kwenye mandhari ya mashambani yaani nyumbani yalimsaidia mara kwa mara alipokuwa shuleni. Tunaendelea kupata tukio jingine alipokuwa kidato cha nne wakati walipokuwa na Kate alipokumbuka kauli moja alilopewa na mamake akiwa nyumbani "Jifya moja halijiki chungu na kidole kimoja hakijasibu kuvunja chawa bado." (uk 123).

Kauli hili lilimsaidia sana katika maisha yake ya shuleni kwani alitambua umuhimu wa kufanya kazi pamoja na wenzake hasa kwenye nyanja ya masomo. Tunamwona akiwa na moyo wa kusaidiana na Kate mwenzake ambaye anatufichulia kuwa Kate alikuwa hodari katika somo la hisabati ilhali naye alikuwa hodari katika fasihi. Wote wawili hamkuwa na yeyote aliyewashinda katika masomo hayo. Kwake Susan anaona infaa wasaidiane kwa lile somo mwenzake hakuwa na weledi wa kutosha. Ushauri mzuri wazazi wake walioutoa kule nyumbani ulikuwa wa msaada sana katika maisha ya Susan hasa alipokuwa skulini. Mchango huu ulimwathiri Susan kwa njia nzuri katika maisha yake hasa alipokuwa mbali na wazazi wake.

Tukio jingine linalotufafanulia jinsi mafundisho ya wazazi wake yalivyomwongoza kufanya uamuzi katika maisha yake akiwa mbali na nyumbani ni wakati alikuwa anaenda nyumbani baada ya kumaliza mtihani.

Mchuuzi mmoja alimjia akitaka kumuuzia pambo fulani pale kituoni mwa magari akingojea gari. Alifanya uamuzi kwa haraka kuwa hangenunua pambo lile kwa sababu aliyakumbuka mashauri fulani aliyopata nyumbani. Susan anatueleza hivi,

> Niliutazama tu sikuuchukua. Nilikumbuka Roselyn alivyopigwa na baba kwa sababu ya kuvaa ushanga tu. Baba alishikilia kuwa mapambo ya aina hiyo hayakuwa ya kikristo. Hayakufananisha na makoa na misiwe iliyovaliwa na wacheza ngoma za kienyeji, wakala wa shetani, kama alivyowaeleza. (uk 125).

Hata ingawa Susan hakukubaliana na dai hili, kwa upande mwingine yalimsaidia kutotumia hela kidogo za matumizi yake ambazo hupewa kwa njia isiyofaa kama vile kununua mapambo. Haya ni matokeo ya athari ya mafundisho ya nyumbani. Kwa yakini mafunzo haya yalimpa mwongozo katika maisha.

Susan alipomaliza mtihani wake wa mwisho na akawa anaelekea nyumbani alipata rafiki mzuri aliyekuwa tayari kumshindikiza huku akimsaidia baadhi ya mizigo aliyokuwa nayo. Baada ya kutoka kwenye gari alipofika karibu na kwao, Susan alimruhusu rafiki ya Cedric Mwambe kurudi asifike nyumbani ili wasionekane na baba yake na kusababisha ugomvi. Ilimbidi kulibeba sanduku lake na mkoba wake pekee hadi nyumbani.

Susan anatuambia hivi: “Alinisaidia kubeba sanduku langu lakini hakufika nyumbani kwenyewe bali aliniaga karibu na ule mkuyu ulioko upande wa chini katika mji wetu. Sikutaka aonekane na baba. Nilichelea maneno ya baba, sikutaka kuaibishwa mbele ya msoni huyu…..” (uk 128). Hii ni athari hasi kwa sababu haikuwa vibaya Susan kusaidiwa mpaka nyumbani hasa wakati huo kulikuwa na giza ambapo alihitaji msaada.

Tukio jingine ambalo tunalipata Susan akiwa chuo kikuu ni wakati alitembelewa na rafiki wake mmoja aliyejitambua kama Zachary Bosire aliyedai alikuwa rafiki wake Alexina. Huku wakimngoja Alexina kurudi Bosire alileta mjadala fulani kuhusu maisha ya Ukristo. Susan aliona kufuru mkubwa kijana huyu alipotoa kauli fulani kuwa, mengi yaliyopo katika Biblia ni sehemu ya fasihi ya kimapokezi ya mataifa ya Mashariki ya Mbali. Susan anasema kuwa baba yake angesikia haya angemuomba Mungu kumwadhibu huyu kijana huku akiitakasa roho yake ya kishetani iliyomjaa Bosire. Anasema Bosire alistahili adhabu kali mithili ya waasi wa Sodom na Gomorah.

Tokeo hili linatuonyesha kuwa Susan aliheshimu Biblia jambo linalopatikana kwao nyumbani na ambalo ni baadhi ya mafundisho ya baba yake na mapenzi yake pia. Tunaipata tofauti kubwa kati ya Bosire jinsi anavyochukulia Biblia na vile Susan anavyoichukulia pia. Mazungumzo zaidi yalikatika hapo hapo na Bosire akaondoka hatimaye. Susan alishangazwa na jinsi ambavyo wanafunzi wengi hawakuwa na imani dhabiti kuhusu dini. Alilazimika kuwazoea tu.

Tunaona athari ya mafundisho ya Biblia ya baba yake bado yakimtawala hata akiwa shuleni. Hali hii ilimsaidia kuwapima wanafunzi wenzake na kujitenga na wale waovu.

Mandhari haya ya mashambani na hasa katika uhusika wa Susan na baba yake tunagundua kuwa wanaume wanawakandamiza wanawake. Jambo hili linajitokeza wakati Susan analalamika kuwa jamii yao imekuwa ikimdharau mwanamke. (uk 196).

Susan anaendelea kusema kuwa jamii hii imebakia mtumwa na mawazo ya kizamani. Aidha anasema lazima watu waelewe mambo yamebadilika sio kama zamani na wakati umepita wa kupokea maagizo bila kudadisi.

Mandhari haya yametuonyesha jinsi ambavyo Richard ameendeleza msimamo wake wa dini. Aidha yanatuonyesha jinsi ambavyo ameathiriwa na utamaduni wa jamii yake.

### 3.4 Mandhari ya shuleni

Mandhari ya shule yalimfanya Susan kupata marafiki. Hawa walikuwa Bethsheba, Dora na Eunice. Siku moja Dora alipendekeza wote waende wakatembee. Bethsheba na Eunice walikumbaliana na wazo lenyewe lakini Susan alipinga wazo hilo kwa sababu aliogopa kukutana na baba yake. Alikumbuka mambo waliofundishwa na baba yao. Baada ya majadiliano waliamua kwenda kutembea. Mpango huu ulikuwa kinyume na mapenzi ya wazazi ndipo tunaona Susan akisitasita lakini kwa sababu ya msukumo wa wenzake mwishowe anakubali. Inaonekana walimu walikuwa wanafanya wajibu wao kwa sababu tunampata Dora akilalamika kuwa walichapwa kwa sababu ya makosa madogomadogo kama kuongea lugha ya mzazi.

Katika mazungunzo yao Dora anamuliza Susan kama alikuwa na rafiki wa kiume mwandishi anatueleza kuwa swali hili lilimshangaza Susan sana. Nyumbani Susan alishauriwa urafiki wa wavulana ulikuwa hatari. Hivi ndivyo anajitetea baada ya swali lile.

Tunambiwa kuwa Susan alishindwa na kueleza alivyoshauriwa na mama yake kuwa lazima ajihadhari na wavulana (uk 19). Hali hii ilimfanya achekwe na rafiki zake kuonyesha kuwa rafiki zake tayari uhusiano wao na wanaume haukuwa jambo geni. Tunaambiwa alikuwa akijiona mjinga kwa kutojua wanaume. Mpaka hapa tunaona Mandhari ya shuleni ambayo ina wanafunzi wenye tabia mbalimbali yameanza kumwathiri Susan kwa kumletea mawazo ya mambo aliyofundishwa nyumbani kuwa yalikuwa kinyume na mafundisho ya Biblia. Baada ya Susan kukaa chuoni kwa muda na pia baada ya kuhusika katika mijadala tofauti na wanafunzi wenzake, hasa Bosire aliyemtembelea chumbani ameanza kuona kama kuna upungufu katika maisha ya dini.

Maisha ya chuoni yameanza kutikisa imani yake hasa jinsi ambavyo baba yake alivyoichukua nguvu ya sala. Susan anatwambia hivi, “Lazima nikiri kuwa uhalisi huu mpya ulishaanza kutikisa kwa nguvu misingi ya imani yangu. Nilishaanza kuuona upungufu mkubwa uliokuwapo katika mwito wa baba kuhusu nguvu na satua ya sala. Lazima yalikuwapo mambo ambayo yalihitaji kukabiliwa kwa namna tofauti.” (uk 145,146).

Tukio lingine linalokaribiana na hili ni kuwa Susan anatwambia kuwa tangu aingie chuoni watu walianza kusema kuwa ameharibika. Awali alikuwa mwenye haya lakini wakati huu hakuwa na haya. Aidha Susan anatwambia kuwa mama yake alishamwambia kuwa alianza kuzembea kazi ya Mungu. Susan anaendelea kusema kuwa baada ya kudadisidadisi masuala ya dini alipata kuona kuwa kulikuwa na shida kwenye dini kuhusiana na msimamo wake kumhusu mwanamke. Yaani mama yake alikuwa mtumwa wa baba yake na hata hakutaka kubisha lolote. Matukio haya mawili yanatuonyesha Susan akiathiriwa na maisha ya chuoni.

Alianza kushuku mafundisho ya Biblia na msimamo wa dini katika masuala fulani. Tunaendelea kuelezwa kuwa Susan akiwa chuoni hasa akiwa mwaka wa pili alipata kuona mengi yaliyomfanya kuanza kuona kuwa, nguvu ya sala kama alivyofunzwa nyumbani haikufaa kusuluhisha matatizo yote katika maisha. Tunaambiwa kuwa mjini ambako chuo kilikuwa kulikuwa na raha ya kila aina pia maisha ya uasi yalikuwa kwa wingi. Susan anatwambia hivi: "Hali iliyokuwapo ilihitaji mageuzi makubwa ya kijamii na hili halikuwa suala la nguvu ya sala" (uk 184).

Hili linaonyesha kuwa wakati huu Susan ameanza kushuku misimamo mikali ya kuamini nguvu ya sala kama alivyofundishwa nyumbani na baba yake. Baba yake Susan hangetarajia hayo yanayompata mwanawe.

Mabadiliko makubwa sana yamwandama Susan hasa kuhusiana na mambo mengi aliyofunzwa nyumbani. Tunaelezwa wakati fulani Susan wakiwa na Roselyn wanamweleza mama yao kuwa wakati umepita wa kufuata mambo hasa ya utamaduni bila kudadisi vyema kuwa wakati umefika wa kuchuja mambo yote. Isitoshe si vyema na haiwezekani kufuata kila kitu tu kumpendeza baba yao au kutomuaibisha. Susan anatueleza haya,

> Lakini ni kweli mama utamaduni huo huo ndio unaowafanya wanawake wasipende kujiendeleza, unawadharau na kuwadunisha. Mama wakati tulionao ni tofauti kabisa na wakati wenu na lazima tuwe na tabia ya kuchuja mambo yote. Hatuwezi kufuata kila kitu tu kumpendeza baba au kutomwaibisha, nilisema. (uk 187).

Dondoo hili linatufunulia adhari zinazoletwa na maisha ya shuleni katika maisha ya wahusika hawa wawili.

Susan anaendelea kulalamika kuwa baba yake alishindwa kwenda na wakati ili kuweza kuelewa watoto wake. Shida yake ililetwa na jinsi alivyobobea katika imani yake. Kwake kilichokuwa muhimu ni kufuata mafundisho ya dini na kuidhamini sana nguvu ya sala. Jambo ambalo lilimfanya ashindwe kuangalia mambo katika uhalisia wake.

Susan haoni manufaa sana katika mafundisho ya dini kama hapo awali. Haya yanatokana na kuathiriwa na maisha ya chuoni. Maisha ya chuoni yamebadilisha mtazamo wake katika mambo mengi. Kuna wakati alimwambia kuwa watu wamekosa imani na dini ya baba yake. Huu ni wakati babake alimfukuza mwanawe Roselyn kwa dai kuwa alikuwa mjamzito. Susan anaongeza kuwa imani inayovunja mji haifai kamwe.

Tukio la Roselyn kufukuzwa nyumbani baada yake kupata mimba, Susan alipinga jambo hili vikali. Susan anamwambia baba yake kuwa kumfukuza Roselyn si hatua nzuri.

Aidha alimwambia kuwa kumfukuza Roselyn hakungesuluhisha lolote na wala tendo hili haliwezi kuondoa aibu. Hakuogopa kusema kuwa kama kulikuwa na makosa ya Roselyn kupata mimba makosa yalikuwa katika malezi yaliyotoka kwenye malezi yao kwa watoto. (uk 196). Mandhari ya chuo kikuu yamempatia Susan ukakamavu wa kujibizana na baba yake aliyekuwa ameogopwa na familia yake kwa muda mrefu.

## 3.5 Hitimisho

Katika sura hii tumechunguza mandhari ambayo ni kipengele cha fani. Mandhari huwa na athari kubwa kwa wahusika wa fasihi. Tumechunguza mandhari ya mjini na jinsi ilivyoathiri wahusika wake. Tumechunguza Richard akiwa mjini Machakos ambako alikuwa akisomea. Shule yake ilikuwa karibu sana na mtaa wa Swahili ambako kulikuwa na kila aina ya shughuli.

Tumeeleza pia kuwa chumba alimoishi kilikuwa kati ya vyumba vingine ambavyo vilijaa kelele ambazo hazingemkubalia kupata nafasi murua ya kutafakari kuhusu masomo. Kuna uwezakano mkubwa kwamba hali hii ilichangia kutofanya kwake vizuri katika masomoni. Aidha alipomaliza shule alienda mjini Nairobi ambamo tunamkuta katika mandhari ya Uhuru Park ambamo aliwapata wahubiri waliomfanya kukata kauli ya kuwa mfuasi wa dini. Alipopata familia alitumia mafundisho ya Biblia kuongoza familia yake. Pamoja na mandhari ya mashambani ambako kulikuwa na athari ya utamanduni ambao hukumpa mwanamke uhuru.

Mwisho tumeangalia mandhari ya shuleni. Mandhari haya yamemwathiri Susan kutaka kuwa na uhuru ambao aliona haukuwa mwao nyumbani. Anakabiliana na baba yake hasa wakati Roselyn dada yake alifukuzwa kwa sababu ya kupata mimba. Alisisitiza kuwa utamaduni ambao haumpi mwananke heshima hauna nafasi kamwe.

Tunamwona baba yake akijirudi na kumwita Roselyn kurudi nyumbani. Utendakazi wa mandhari katika *Nguvu ya Sala* umedhihirika kibayana kutokana na hali hizo tofauti ambazo wahusika wanajipata na namna zinavyowaathiri.

# SURA YA NNE

# SWALA LA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA *NGUVU YA SALA*

## 4.1 Utangulizi.

Kwenye sehemu hii tutashughulikia kipengele muhimu sana ambacho ni wahusika. Kipengele hiki kimetumika kukuza maudhui ya *Nguvu ya Sala.* Mwandishi ametumia wahusika mbalimbali wakiwemo wazazi na watoto wao. Wahusika wakuu ni Richard Ngunze na bintiye Susan Nzisa. Kisa hiki pia kinahusisha Mary Kasiva na watoto wao wengine.

Katika riwaya hii kuna wahusika wakuu, wahusika wadogo na wahusika wajenzi. Baadhi ya wahusika wamejidhihirisha kama wahusika wa kimviringo ilhali wengine ni wahusika bapa ambao hawabadiliki sana. Wahusika hawa wanatumiwa na mwandishi kuiendeleza hadithi yake.

## 4.2 Wahusika wakuu katika *Nguvu ya Sala*

Katika sehemu hii tulishughulikia wahusika wakuu. Wahusika wakuu katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* ni viumbe ambao wanapatikana kutoka mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Mwandishi ametumia wahusika hawa katika kukuza kisa chake na pia wameelezwa kwa kina. Madumulla (1991) anasema kuwa matendo na wasifu wa mhusika mkuu yanachukuana na hali ya kawaida (ya kila siku) ya maisha ya jamii, na ambaye matakwa yake na malengo yake kwa namna fulani, yanaoana na kilio cha walio wengi na kudhihirisha hofu na matumaini yao.

Naye Mbatiah (2001) anasema mhusika mkuu huonekana wazi kuwa ndiye nguzo ya msimulizi kwa kuwa ndiye muhimu kuliko wengine wote. Anahusika na matukio makuu ya hadithini. Wahusika wengine wanahusishwa naye na wanasaidia kumjenga.

Wataalamu hawa wote wanakubaliana kuwa, kuna mhusika mkuu na majukumu yake ni muhimu kutupatia ujumbe katika kazi ya fasihi. Katika *Nguvu ya Sala* wahusika wakuu ni Susan Nzisa na Richard Ngunze.

### 4.2.1 Susan Nzisa

Susan Nzisa ni mmoja wa wahusika wakuu. Mhusika huyu anatawala riwaya hii kutoka mwanzo mpaka mwisho. Susan Nzisa ndiye kifungua mimba katika familia yao na nyuma yake kuna wasichana watatu ambao ni wadogo wake. Susan anatueleza, "Mimi ndiye niliyekuwa kifungua mimba. Aliyenifuatia ni Roselyn naye akafuatwa na Jacquiline" (uk1). Watoto wote wanne walikuwa wasichana. Wazazi wote wa Susan walikuwa hai. Susan alikuwa msichana mwerevu kwenye masomo yake na alipenda masomo. Tunaelezwa na Susan,

> Ndoto yangu ilishakuwa kweli na nina furaha
> ghaya matokeo ya mtihani yalikuwa mazuri.
> Mimi ndiye niliyekuwa mwanafunzi bora katika
> shule yetu. (uk. 30).

Kutokana na bidii yake shuleni aliweza kujiunga na shule ya upili ya wasichana ya Miwani mjini Machakos. Mhusika huyu alikuwa shupavu. Tunamwona akibishana na baba yake baada ya babake kumfukuza Roselyn.

Sababu ya Roselyn kufukuzwa ilikuwa kupata mimba akiwa bado shuleni. Babake Susan aliogopwa sana na kila mtu nyumbani lakini hili haikumzuia kujibizana naye. Tunaambiwa yafuatayo,

> Baba, kufukuza  Roselyn sio malezi
> Nilimjibu.Unasema nini?Alikuja juu
> Baba huku midomo yake ikianza
> Kumchezacheza.......Kumfukuza Roselyn
> Hakusuluhishi lolote wala sio njia ya
> Kuondolea aibu, nilisema……. Hayo
> ni mawazo mabaya baba….(uk 196).

Majibizano haya yaliendelea kwa muda mrefu. Hatima ya majibizano yenyewe yalimfanya baba Susan kutulia na kubadili msimamo wake. Tunamkuta akitumana Roselyn aitwe arudi nyumbani. Susan alikuwa mdadisi. Alipenda kujua na kufahamu mambo. Hii ni sifa nzuri hasa kwa wanafunzi. Alitamani kufahamu kwa nini mambo yawe jinsi yalivyokuwa. Hii ni sifa ambayo hatujaiona kwa mhusika mwingine. Tunasoma hivi,

> Mama, mwalimu alisema kuwa kuna shujaa
> fulani aliyezikwa kwenye pango fulani kijijini.
> Je,ni kweli? Alisema kuwa kuna mashujaa
> wengi wa jamii yetu: Masaku,Syondonga na
> Syokimau. (uk 9)…
> Pia kuna ubaya gani mama
> kucheza? (uk. 2).

Susan aliuliza maswali haya aweze kuelewa. Tunamkuta tena akimuuliza sista Emily ”je, sista umefanya kazi yako kwa miaka mingapi?” (uk. 64). Susan alizingatia mashauri ya wazazi wake wakati wote. Hali hii ilimfanya kuwa mtoto mzuri katika maisha yake. Tunasoma hivi, “Niliyakumbuka maneno ya mama kuwa njia pekee ya kumfurahisha ni kwa kupita mtihani wa kidato cha nne na kufuzu kujiunga na chuo Kikuu.” (uk 90).

Maneno kama haya yalimtia moyo katika masomo yake na hata katika maisha yake kwa jumla. Susan alikuwa mhusika mwerevu shuleni. Walipofanya mtihani wa kidato cha nne alikuwa mmoja wa wale waliokuwa wamefanya vizuri sana. Hii inaonyesha kuwa alikuwa mwenye bidii katika masomo yake. Tunaelezwa hivi, “Matokeo ya mtihani wa mwigo yalishatoka sasa. Nilikuwa mwanafunzi wa pili katika orodha ya wanafunzi kumi bora”(uk 119). Susan ametumiwa na mwandishi sana katika kazi hii, vile vile amejengwa kwa kina, hivyo basi ni kweli kuwa mhusika huyu ni mmoja wa wahusika wakuu katika riwaya hii.

### 4.2.2 Richard Ngunze

Mhusika huyu ndiye aliyekuwa baba yake Susan. Richard alitambulikana kama mwenye misimamo dhabiti kuhusu dini. Tunaelezwa,

> Alifahamika kijiji kizima. Wazee wa
> kijiji walimwelewa na kuielewa misimamo
> yake.
> Baadhi yao walimchukia na
> kuikashifu misimamo yake hiyo lakini
> hakujali wala kubali. (uk 5).

Hata ingawa watu walimwelewa kwa misimamo hiyo sio wote walioona akiwa na maisha mema kutokana na misimamo yake. Richard alikuwa mwanamume wa makamo na mpole. Richard alijulikana kwa sifa hii. Tunaelezwa na mwandishi, “Alikuwa mwanamume wa makamo. Umri wake ulikuwa miaka arobaini na saba…. Hakuwa msemaji sana.” (uk 5).

Richard alikuwa dikteta, yaani alitawala kimabavu. Sifa hii inafanya aogopwe sana na bibi yake ambaye anaonekana kujitenga bali katika kutoa adhabu kwa watoto pindi anapowapata na hatia. Sifa hii inaonekana katika malezi ya watoto wake. Mara angepata maagizo yake hayakufuatwa, alitoa vita. Tunaelezwa na mwadishi haya, “Siku hiyo jioni baba alinipiga sana.” (uk.2)

Huu ni wakati Susan alienda kucheza na watoto wa jirani ambao hawakuwa wakristo jambo ambalo lilikuwa limekataliwa. Susan anaeleza, “Nilimwogopa baba kuliko nilivyomwogopa mwalimu.”( uk. 4) Richard Ngunze alikuwa jasiri alipokanywa kukata mkuyu na mzee fulani kutokana na kuwa ilikuwa hatari kukata mkuyu huo, yeye aliamua kuukata. Tunasoma kuwa alipoanza kukata na baada ya kumegua kipande cha mti, nyoka mkubwa alitokea. Tunasoma yafuatayo:

> Aliliinua lile shoka na kuliachilia kwa nguvu. Lilimegua kipande kidogo cha mti ule; kigamba cha mti ule tu…
> Alikuwa hajaachilia alipomwona nyoka mkubwa akitambaa na kunyiririka kuelekea alipokuwa amesimama.(uk 7, 8).

Kutokana na dondoo hili, Richard hakufungwa na utamanduni wa wakati wake. Richard alikuwa mhusika mkali. Aliwapa watoto wake vichapo walipokosea. Aliiona njia hii kama iliyofaa kuitawala familia yake. Tunasoma kuwa, "Alitokeza baada ya dakika chache mikononi kashika bakora yake na kuanza kumcharaza huku akimwapiza." (uk 193). Hali hii ilitokea baada ya kuelewa kuwa Roselyn amemuaibisha kwa kupata mimba akiwa shuleni na kuaibisha kiongozi wa dini.

Mhusika huyu pia ana sifa za mhusika wa kimviringo kwa sababu tunamwona akibadilisha msimamo wake wakumrudisha Roselyn nyumbani baada ya mabishano makali kati yake na Susan. Mhusika huyu na uhusika wake unaipa riwaya hii mvuto wa hali ya juu sana. Uhusika wa Richard Nguze ni wa uchangamano. Awali alikuwa mtu wa kawaida na masuala ya kidini hakuyajali sana. Baadaye anapoanza kuzingatia dini anaishikilia kwa nguvu na kuitumia kama kurunzi ya kuongoza familia yake. Jambo hili linamfanya kuwa mkatili dhidi ya famila yake

Bintiye Susan anamfanya kulegeza msimamo wake anapotetea dada yake aliyepata mimba na kufukuzwa nyumbani. Richard anakubali arejee nyumabani.

### 4.3. Wahusika wadogo

Katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* wahusika wadogo wamegawanyika katika makundi mawili. Kuna wahusika wajenzi ambao wanatusaidia kuwaelewa wahusika wakuu. Wahusika hawa ni: watoto wa Richard Nguze na Mary Kasiva nao ni, Roselyn na Redemta na Jacquiline. Wahusika wengine ni wahusika wasaidizi ambao wanamsaidia mwandishi kukuza maudhui ya riwaya hii. Wahusika hawa ni, Bethsheba, Octavian Birundu, Sista Emily, Manyara na mkewe na mwisho Rose Mafali.

### 4.3.1 Mary Kasiva

Mhusika huyu alikuwa bibi yake Richard aidha mama yake Susan. Uhusika wake haujatawala nafasi kubwa kama wahusika Richard na Susan. Mhusika huyu alikuwa mke wa nyumbani. Sifa moja yake ni kuwa alikuwa mnyonge sana.

Sifa hii tunaipata wakati watoto wake wanachapwa na baba yao. Ndani yake alionekana kutofurahishwa na adhabu hiyo kali lakini alikaa kuangalia tu. Jambo ambalo hata watoto wake waligundua. Tunaelezwa,

> Alinicharaza kwa mshipi. Nililia kwa sauti
>
> lakini haikunisaidia. Aliendelea kunipiga.
> Wadogo wangu walianza kulia. Vilio
> vilikuwa vya kupokezana siku hiyo.
> Mama alishindwa kutusaidia. (uk. 3).

Hali hii mara nyingi hupatikana kwenye hali ambazo utawala ni wa kimabavu kiasi kwamba akina mama wamedharauliwa na kunyimwa uwezo wa kutawala.

Susan alipoenda kucheza na watoto jirani mamake anamwambia haya, “Kucheza si kubaya lakini amekukataza baba yako kucheza na watoto hao”. (uk 2). Maneno haya yanatuonyesha kuwa yeye haoni ubaya wa kucheza na wenzao lakini kwa sababu mumewe amekataza basi naiwe hivyo. Mama Susan alionekana kujitenga na makosa ya watoto wake. Alitakiwa kuchukuwa hatua pale pale. Mary Kasiva alikuwa mrembo. Alikuwa na umri mdogo kuliko mumewe. Mhusika huyu alikuwa na sifa ya uvumilivu. Sifa hii ilimwezesha kuishi na mumewe aliyeishi naye maisha ya kukandamizwa.

Mary Kasiva aliwahi kuchapwa hata kovu fulani likaachwa mwilini wake. Haya yote hayakumfanya kufikiria kutoroka kutafuta maisha huru. Aidha Mary alikuwa mnyenyekevu katika maisha yake. Sifa hizi mbili zinamsidia kuishi na mumewe. Mhusika huyu alishikilia utamaduni na itikadi zake.

Mumewe alipokatazwa kuukata mkuyu na mzee fulani, mhusika huyu anamsihi kutii. Tunasoma hivi, "Mkewe alipoelewa dhamira yake alimkataza Kwa kumsihi ayafuate mawaidha ya yule mzee aliyemsihi asiuguze". (uk 7). Richard hakusikia mashauri ya mzee wala ya mkewe bali alimwona mkewe kuwa binadamu dhaifu.

Mary Kasiva anawakilisha wahusika wa kike ambao wanajikuta katika taasisi ya ndoa ambayo ni kero kwao. Anadhulumiwa pia watoto wake wananyanyaswa lakini hana uwezo wa kukabiliana na hali hii.

### 4.3.2. Roselyn

Mhusika huyu alikuwa mtoto wa pili wa Richard Ngunze. Alisoma shule ya msingi hata kuendelea na masomo ya shule ya upili.

Roselyn hakuwa na maadili mema. Alipata mimba akiwa bado shuleni jambo linalotufahamisha kuwa alishiriki mapenzi kiholela akiwa bado shuleni. Tunaambiwa hivi, "Umefukuzwa shule? Kwa sababu gani? Aliuliza mamake "kwa sababu ya …a…mimba, alisema Roselyn." (uk 192).

Hili ni jambo lililoleta aibu kuu katika familia ya Ngunze. Aidha, tunafahamu kuwa alikuwa akiendesha maisha ya mapenzi kisiri bado akiwa shuleni jambo ambalo hakuna aliyefahamu hadi alipofukuzwa na kuja nyumbani.

Mhusika huyu alipenda raha. Mara kwa mara alipenda kusikiliza muziki kutoka redioni. Tunaelezwa hivi, “Nilirudi nyumbani na kumkuta Roselyn akicheza muziki”. (uk 113).

Roselyn hakuwa mfuasi wa dhati wa mafundisho ya Biblia. Hakupenda kuzingatia matakwa ya babake. Roselyn alikuwa na msimamo wa kutojali. Sifa hii tunaipata wakati alichelewa baada ya kuumaliza mtihani.Alipoulizwa na mamake, jibu alilotoa lilionyesha udhaifu huu,

> Hivi siku za mtihaniziliongezwa? Aliuliza
> Mamasiku hiyo. Mtihani uliisha jana
> asubuhi alisema Roselyn.
> Wakati huu wote ulikuwa wapi?
> Niliambatana na rafiki yangu,
> Alisema Roselyn kwa ukakamavu. (uk 186).

Kulingana na dondoo hili Roselyn ameacha kuogopa babake ambaye amemwogopa kwa muda mrefu. Roselyn haoni kutembea kwa rafiki zake kukiwa na tatizo lolote. Hata baada yake kupata mimba alionyesha hali hii ya utovu wa nidhamu.

### 4.3.3 Bethsheba

Bethsheba alikuwa mhusika mwenye huruma na rafiki wa Susan. Susan alipokuwa mgonjwa na kuwa kwenye bweni peke yake, Bethsheba alikwenda kumtuliza na kumpa pole. Tunaelezwa;

> Nilikuwa peke yangu. Bethsheba alitokeza
> upande wakusini, akitokea bweni la
> Kilimanjaro, bweni letu …….

> Nilikuwa bado nashikilia tumbo langu ingawa
> sikumwita alitambua hili. (uk 59).

Mhusika kama huyu ni wa maana sana kwa sababu wanakuwa wa msaada wakati wa shida. Tukikumbuka kuwa wakati kama huu jamaa wa Susan hawakuwa karibu, Bethsheba alichukua nafasi muhimu. Mawazo ya Bethsheba hayakutulia kwa sababu ya ugonjwa wa Susan. Tunasoma hivi, “Bethsheba alitoka darasani saa kumi lakini inawezekana alitoka mapema zaidi. Alipofika bwenini alikuta nimelala.” (uk 65). Bethsheba alikuwa mzembe. Mhusika huyu hakutia bidii masomoni hivyo hangefanya vizuri kama rafiki zake,

> Bethsheba alikuwa nambari ishirini na
> mbili. Yeye hakujali sana. Alishanielezea
> mara kadha wa kadha kuwa hakuwa na
> nia ya kuendelea na masomo yake.
> (uk 119).

Bethsheba alitawaliwa na mawazo kuwa wanaume ndio waliostahili kusoma kwa sababu majukumu ya nyumbani yalikuwa mikononi mwao.

Msimamo huu haukuchukuliwa na Susan kama wa kweli. Susan aliamini kuwa jinsia zote ni sawa, kwa hivyo hata wanawake walikuwa na nafsi sawa ya kujiendeleza kimasomo.

### 4.3.4 Octavian Birundu

Mhusika huyu alikuwa mwalimu shuleni mwa akina Susan. Alikuwa mwalimu wa somo la Sayansi na alifunza Susan somo hilo. Aidha, alikuwa mkuu wa kundi la uigizaji shuleni. Mwalimu Birundu pia alikuwa mshauri wa wanafunzi.

Mhusika huyu hakuwa mwadilifu. Kulikuwa kumepitishwa sheria shuleni kuwa wanafunzi wasipatikane nyumbani kwa waalimu kamwe. Tunamwona Birundu akimtuma mwanafunzi fulani kumwita Susan aende nyumbani kwake. Tunasoma kuwa,

> Naikumbuka siku hiyo vizuri…. Ulikuwa wakati kama huu wa leo tu. Mwanafunzi mmoja wa kidato cha kwanza alinijia na kuniarifu kuwa natakiwa na mwalimu wa sayansi, Octavian Birundu.(uk 67)

Udhaifu wake unadhihilika kabisa kwa kuwa alielewa fika kuwa, sheria ilisema vizuri sana kuwa wanafunzi hawakuruhusiwa kupatikana kwa walimu hususan wa kiume ilhali yeye alimwita Susan kwake nyumbani. Tunasoma hivi,

> Licha ya kuwepo kwa sheria hiyo wanafunzi walizitembelea nyumba za walimu wa kiume. Walimu waliofuata sheria hiyo kwa dhati walikuwa wawili tu: mwalimu mkuu na naibu mwalimu mkuu. (uk 68).

Hapa tunaona mwalimu Birundu hakuwa kielelezo chema licha yake kuwa mshauri wa wanafunzi. Ilifaa awe mfano mwema kwa kutii sheria za shule. Tunaelezwa wakati fulani Susan alilalamika kwa sababu ya mwalimu huyu. Siku moja Birundu alimshika Susan mkono kwa nia ya kutaka mapenzi.

Susan alikataa shinikisho hili kwa kusema, "Mbona unanishika mkono wangu?" Nilliuliza kwa hasira. (uk 79). Octavian alikuwa na sifa mbaya ya kuwa mwasherati. Mwalimu huyu hakuwa mwaminifu aliwadhulumu wasichana wachanga kimapenzi.

Tunafahamishwa kuwa alihusika katika kashfa ya kumtia msichana wa shule mimba jambo ambalo lilimfanya kufutwa kazi. Tunasoma hivi,

> Nimesikia kuwa mwalimu Octavian Birundu
>
> ameachishwa kazi. Alisema Bethsheba. …..
>
> Kuna gani tena kamtia mimba mtoto wa
>
> watu, alisema Bethsheba. (uk 139).

Mhusika huyu hakufaa katika kazi aliyopewa shuleni yaani kuwa mshauri wa wanafunzi. Mwandishi anamtumia mhusika huyu kupitisha ujumbe kuhusu maadili katika kazi. Ni bayana kuwa Octavian Birundu anatumiwa na mwandishi kuonyesha jinsi baadhi ya walimu wanakaidi maagizo na kuishia kuwa watu wasiotegemeka badala ya kuwa vielezo kwa wanfunzi.

### 4.3.5 Sista Emily

Mhusika huyu alikuwa mhudumu katika dispensari ya shule. Sista Emily aliipenda kazi yake. Aidha aliwajibikia kazi yake. Haya tunapata kwenye dondoo hili,

> Nilifurahi kuwa na Sista Emily. Alinielewa nami
>
> nilijitahidi kumwelewa. Labda wakuu wa shule
>
> walifahamu kuwa alikuwa Sista wa kutegemewa.
>
> (uk 62).

Dondoo hili linatundokezea kuwa mhusika huyu alipendwa na wateja wake waliokuwa wanafunzi wake. Pia tunasoma haya: "Alipendwa sana na wale wasichana wakubwa. Aliingiliana nao vizuri……Fortunata alikuwa mmoja kati ya wasichana waliopatana na Sista Emily kwa uzuri."(uk. 64).

Hakufuata mfumo wa maadili kama mhudumu wa dispensari. Katika mazungumzo kati ya Susan na Bethsheba wakiwa hotelini, tunafahamu kuwa mhusika huyu alimsaidia mwanafunzi mmoja kuavya mimba jambo ambalo halikuwa nzuri. Kitendo hiki kilimfanya afutwe kazi kama mhudumu wa dispensari ya shule. Tunasoma hivi,

> Alitafuna kwa muda kisha akaongeza nasikia
> kuwa hata Sista Emily ameachishwa kazi pamoja naye.
> Yule mhudumu wa dispensari ya shule?
> Niliuliza…..Nasikia alijaribu kumsaidia yule binti
> Kuitoa ile mimba ya Octavian, alieleza
> Bethsheba. (uk. 140).

### 4.3.6 Redemta na Jacquiline

Wahusika hawa walikuwa dada zake Susan. Redemta ndiye aliyekuwa kitinda mimba naye Jacquiline ndiye aliyekuwa mkubwa wake kwa umri. Dada hawa walikuwa watoto watiifu kwa wote. Mara nyingi ndio waliokuwa wakitumwa. Tunasoma hivi, "Aliyenifuata ni Roselyn naye akafuatwa Jacquiline, kitinda mimba alikuwa ni Redemta". (uk 1).

Watoto hawa walipendwa sana na baba yao. Mapenzi ya baba yalikuwa kwa Redemta kwa wingi.

Alihakikisha kuwa aliyetumwa lazima Redemta angeandamana naye. Tunasoma haya hapa, "Jacquiline alishatumwa sokoni na baba na aliandamana na Redemta. Hii ndiyo iliyokuwa sheria ya baba; kila atakayetumwa mahali lazima aandamane na Redemta aliyependwa sana na baba kama mboni na jicho" (uk. 105,106). Richard alikiri kuwa Redemta ndiye aliyekuwa na tabia nzuri sana kushinda watoto wake. Redempta alitumiwa na baba yake kama mpelelezi. Alitakiwa kuchunguza tabia za wakubwa wake na kumripotia baba yao. Hii inadhihirisha kuwa baba yao hakuwaamini watoto wake kamwe na hakufikiria wangeweza kuzingatia maadili bila ya kuwawekea sheria kali.

### 4.3.7 Manyara na Mkewe

Deogratias Manyara alikuwa mkurugenzi wa kampuni iliyoitwa *M G Contractors*. Mhusika huyu hakuwa mwaminifu katika ndoa yake.

Tunafahamishwa kuwa alimdhulumu kimapenzi msichana wake wa kazi. Kitendo hiki alikitekeleza alipoachwa na mke wake aliyekuwa mwana biashara.

Tabia hii ilimpelekea yaya kufutwa kazi na mke mtu. Tunasoma hivi, "Mapenzi haya yalitumbukia nyongo baada ya miezi mitatu, Mary aliposhika mimba."(uk. 166).

Baada ya kitendo cha kumpachika msichana huyu mimba, aliamua kumsaidia kuitoa ile mimba akiwa na kusudi la kulificha jambo lile. Mwandishi anatwambia hivi, "Alimweleza Deogratias ambaye alimpeleka kwa rafiki Yake daktari aliyekuwa na kliniki yake mjini na ile mimba ikatolewa."(uk. 166). Mhusika huyu alidhihirisha utovu wa nidhamu. Ni kielelezo kibaya.

### 4.3.8 Rose Mafali

Mhusika huyu ni msichana waliyesoma pamoja na Susan. Rose alikuwa rafiki wa Susan na walihusiana vizuri. Mhusika huyu alipenda sana kuzungumza lugha ya kiingereza kila mara. Tunasoma yafuatayo,

> Naona unajitahidi kuielewa *pythogras theorem*
>
> Alianza Rose ….. *In fact it is better* huko kuna afadhali kabisa.
>
> Aliniunga mkono Rose. …..*Eh … Eh* …
>
> Nilikwenda kumwopoa huko *library,* alisema Rose.Huo mpachiko
>
> itajampa *pressure* tu. (uk. 91-93).

Mhusika huyu aliweza kuiba karatasi la mtihani wa mwigo. Karatasi hili alipenda wajadiliane na Susan ili waupite mtihani wa mwigo "Wakati huo huo Rose alichopoa karatasi fulani ya rangi ya buluu hafifu… hakika ilikuwa karatasi la mtihani wa mwigo."(uk. 96).

Rose hakuwa mwadilifu alipofahamishwa kuwa haifai kutumia karatasi la mtihani lililopatikana kwa njia isiyokuwa halali alisema hata nchi haina watu wengi wenye maadili.

Tunasoma hivi, "Susie, wanaozifuata sheria hizo au wanaoongozwa na maadili katika nchi hii ni wachache kama wapo…." (uk. 97). Kauli hii ni hakika kuwa mhusika huyu hana maadili mema. Mhusika huyu alikuwa na sifa ya uzembe masomoni.

Matokeo ya mtihani yalidhihirisha vizuri kutokuwa na bidii katika masomo yake. Tunaambiwa hivi katika dondoo hili, "Rose Mafali alikuwa miongoni mwa wanafunzi wa mwishomwisho lakini hakujali wala kubali."(uk. 120).

## 4.4 Hitimisho

Wahusika wakuu katika riwaya hii ni Susan Nzisa na Richard Ngunze. Wahusika hawa wawili wameitawala riwaya hii kutoka mwanzo hadi mwisho. Kama ambavyo tumetaja hapo juu wahusika hawa wanawakilisha vilio vya wengi. Susan anawakilisha watu wale ambao wamenyimwa uhuru katika maisha kwa sababu ya kukandamizwa na walio na nguvu zaidi yao. Hata hivyo Susan anajaribu kukabiliana na baba yake. Susan anaonyesha ushujaa wa hali ya juu. Mhusika huyu katika mwisho wa riwaya tunamwona akifaulu.

Richard naye anaakilisha wazazi wale wanahakikisha watoto wao wamepata malezi mazuri. Mhusika huyu anatumia hata Biblia kuwaelekeza wanawe lakini haonekani kufaulu. Kulingana na E. Forster akinukuliwa na Wamitila (2002) wana sifa ya wahusika duara. Hii ni kwa sababu tumepata mabadiliko katika maisha yao. Tunamwona Susan akilelewa kwenye mandhari ambayo yalimfanya awe na woga lakini tunapokuja mwisho wa riwaya anabadilika na kuwa mkakamavu kiasi kwamba aliweza kukabiliana na babake alipotabua kuwa alikosea.

Aidha, tunaweza kusema kuwa masomo yake yalimsaidia kuona mambo tofauti na alivyoyaona akiwa mdogo na hata kuona mambo tofauti na jinsi wazazi wake walivyoyaona. Tukumbuke kuwa alisoma mpaka chuo kikuu.

Kiwango hiki pia kingemfanya kuona na kusema kama jinsi alivyoyaona mambo. Mhusika huyu anatusaidia kuona kuwa sio nguvu tu ya sala iliyo na majibu ya kila tatizo bali kunazo njia nyingi za kutumia. Anamuuliza babake kwa nini hawakutumia nguvu ya sala kutatua shida za Roselyn mnuna wake alipofukuzwa shule baada ya kupata mimba.

Susan anatusaidia kumfahamu babake kuwa alikuwa mkali hasa mtoto angeenda kinyume cha mapenzi yake. Susan alipata vichapo alipocheza na watoto wa jirani jambo ambalo alikuwa amekatazwa. Alimfanya baba yake ayaone makosa yake baada ya kufukuza Roselyn. Kupitia kwake tunapata kuona uhalisia wa maisha katika jamii. Tunaona jinsi familia fulani hukataza watoto wao kushirikiana na watoto jirani. Aidha, tunaona kufanikiwa kimasomo kwa watoto walio na bidii katika maisha. Aidha tunapata jamii nyingi watoto wasiofuata mashauri ya wazazi huharibikiwa na maisha kama mhusika Roselyn.

Richard Ngunze alipokosolewa na Susan alibadilisha mawazo wakati alimrudisha bintiye nyumbani. Kupitia kwa mhusika huyu tunaona utawala mbaya wa nyumbani. Aidha anamnyima bibi yake uhuru wa kuishi. Wahusika wengine ni wahusika wajenzi ambao wamesaidia kujenga riwaya nzima. Uhusika wa wahuhusika hawa wengine wamehusiana na wahusika wakuu kuendeleza maudhui ya kazi nzima. Mamake Susan ana sifa ya mhusika bapa kwa kiasi fulani kwa sababu hatumwoni akibadilisha namna alivyoishi. Tunatarajia apingane na maisha ya kukandamizwa lakini anaonekana mwenye woga mwingi. Kwa jumla riwaya hii ina uhalisia wa maisha ya jamii ya kisasa.

Katika sura hii tumeshughulikia kipengele cha fani cha wahusika. Tumepata kuwa ni kipengele muhimu sana katika fasihi. Tumeeleza maana ya neno wahusika.

Tumesema kuwa ni 'watu' tunaokutana nao na kutokana na vitendo, mazungumzo yao na maelezo ya msanii tunapata ujumbe wa fasihi. Tumeeleza sifa za wahusika kama zilivyojitokeza. Tumejua udhaifu na uwezo wao. Aidha tumewainisha.

# SURA YA TANO

# MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sehemu hii tutashughulikia matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo. Matekeo ya utafiti yatatusaidia kufahamu kwa hakika kama malengo ya kazi hii yameafikiwa pia kama maswali ya utafiti yamejibiwa. Sehemu hii pia itaangazia mapengo zaidi ambayo yanafaa kushughulikiwa ili kufanikisha mahitaji ya wasomaji.

## 5.2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti

Tumegundua kuwa mwandishi ametumia misuko ya aina mbalimbali katika kazi yake. Tumepata kuna msuko mkuu na kuna visuko vidogo vidogo ambavyo vinaendeleza msuko mkuu kwa njia mzuri kabisa. Msuko mkuu na visuko vingine vina uhusiano wa karibu na hukamilishana vyema. Tumepata kuwa msuko mkuu unahusisha wahusika wawili ambao ni Richard Ngunze na Susan Nzisa. Msuko huu unamchora Richard akiwa mzazi aliyependa watoto wake kuwa vielelezo vizuri katika jamii. Kwa hivyo aliwahimiza wayashike mafundisho ya Biblia wakati wote na watumie nguvu zinazopatikana katika sala inapohitajika.

Tunampata akiwahimiza kukariri mafungu ya Biblia kila wakati. Endapo walikiuka mashauri yake wangepata vichapo. Hakupenda kamwe washiriki michezo na watoto wengine ili kwamba wasiathiriwe visivyo. Bibiye Richard hakupata uhuru katika maisha kwa sababu uongozi wa Richard ulikuwa mkali na hakupata nafasi kubwa ya kuongoza familia yao. Richard alimnyima nafasi hii. Watu kule nje waliona maisha ya familia hii kuwa sawa lakini wenye mji waliumia kiasi.

Susan aliyekuwa mtoto wake alijaribu kuuliza sababu ya mambo fulani lakini hakupata majibu kamili. Kwa mfano alipenda kujua kwa nini wasicheze na watoto wengine. Baada ya Susan kwenda masomoni na kupata uwazi wa maisha alibadilisha misimamo fulani na kuamua kukabiliana na babaye. Tunaona mwisho wa tukio hili mabishano makali yaliyoleta mabadiliko kwenye mtazamo wa Richard.

Mvutano huu unaishia Susan akitaka ieleweke kuwa malezi waliyoyapata kutoka kwa wazazi wao hayakukamilika kwani hawakuelezwa uhalisi wa maisha na pia nguvu ya sala sio pekee suluhisho ya matatizo yote katika maisha. Msuko huu unaleta mgogoro wa wahusika hawa jambo linaloleta taharuki katika kazi nzima. Msuko huu unatufanya kupenda hadithi hii kutokana na mvuto unaopatikana pale. Tunapenda kuisoma hadithi hii mara kwa mara. Msuko huu kwa kiasi kikubwa unafanya tuseme kuwa mwandishi wa riwaya hii amefaulu kuunda sifa nzuri ya fasihi.

Pamoja na msuko mkuu kuna visuko vidogo ambavyo bado mchango wake ni mzuri kujenga kazi mzima hata ingawa mchango ni mdogo. Kwa mfano, tuna kisuko kinachowazunguka Richard na mkewe. Richard anamnyima mkewe uhuru wa kuwaelekeza watoto wake. Haya tunapata tunapotambua kuwa wakati watoto wanapokosea mama yao huwashtua tu kuwa angewastaki kwa baba yao. Tunabaki kujiuliza kwa nini hangewaadhibu pindi alipowapata na makosa. Kati ya wahusika hawa wawili hatupati mvutano wowote na hivyo tukiwaachia kuunda riwaya hii yote basi riwaya nzima haingepata mvuto wowote. Lakini hata hivyo kisuko hiki kinasaidia kusukuma riwaya mbele.

Kuna kisuko kingine kinachohusisha Susan na Octavian Birundu. Huyu alikuwa mwalimu wa Susan. Mwalimu huyu alivunja sheria za shule kwa kuwaalika wasichana wa shule kwake nyumbani jambo lililokuwa limekataliwa na sheria za shule. Tunamwona akimwalika Susan kwake nyumbani lakini mwandishi hajatwambia kilichotokea. Hivyo tunasema hiki ni kisuko kodogo. Pia tuna kisuko kingine kinachomzunguka Richard akiwa shule. Anapata ugonjwa wa kuumwa na kichwa na kwenda nyumbani. Nyumbani anapelekwa kwa mganga na mamaye. Kisuko hiki pia hakina mvutano mkubwa.

Aidha tuna kisuko cha manyara, mkewe na mfanyi kazi wao yaani Mary Kasiva aliyekuja kuwa mkewe Richard Ngunze. Kisuko hiki kina mvutano kati ya Manyara na mkewe. Manyara alikuwa na kashfa ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Kasiva. Jambo ambalo mkewe alikuja kufichua. Tukio hili linaishiakwa Kasiva kufutwa kazi na kwenda zake. Kisuko hiki hakichukui mkondo mrefu hivyo kuwa kisuko kidogo. Visuko hivi na vingine ambavyo utafiti huu ulipata ni dhihirisho tosha kuwa, mwandishi alitumia misuko anwai katika kazi yake.

Utafiti wetu pia umepata kuwa mwandishi ametumia wahusika kukuza maudhui yake. Wahusika waliotumiwa ni wengi na waamegawanywa katika viwango tofauti tofauti. Tulipata wahusika wakuu. Wahusika hawa ni wa maana sana na wanapatikana katika kazi hii kutoka mwanzo hadi mwisho. Mchango wao ni muhimu sana katika maudhui ya kazi nzima. Kwa mfano Richard Ngunze ambaye ni mmoja wao anasawiriwa kama mhusika aliyezama kwenye dini. Ana imani kuu katika dini. Ni muhudumu wa kanisa katika kitengo cha juu. Tunaelezwa yeye alikuwa kiongozi wa kanisa. Aliwahimiza wanawe kufuata mafundisho ya Biblia. Kweli watoto wake walifuata hata ingawa walipokuwa wakubwa walianza kuwa na mashaka juu ya dini. Mhusika huyu aliamini nguvu ya sala ambayo ndiyo anwani ya riwaya hii. Shughuli za dini alizifanya kwa moyo wake wote. Hata majirani walikiri ukweli huu.

Susan alikuwa mtoto wa Richard Ngunze na ndiye aliyekuwa kifungua mimba wa mkewe. Katika maisha yake hadi chuo kikuu, mwanzoni tunamwona akiwa anachukulia mafundisho ya dini vizuri. Hali hii inaonekana kubadilika anapokaribia kumaliza masomo ya chuo kikuu. Susan anadai kuwa nguvu ya sala pekee haiwezi kuleta majibu ya kila hitaji. Pia analalamika kuwa pamoja na utamaduni jinsia ya mwanamke imekandamizwa. Anachorwa akilalamika mbele ya babake kuhusu madai hayo. Tuligundua kuwa ukakamavu huu aliupata chuoni alikopata uwazi wa mambo. Utafiti wetu umegundua kuwa wahusika hawa wawili wamechangia pakubwa sana katika kuunda maudhui ya kazi hii.

Tulipata kuwa kuna wahusika wajenzi. Hawa wanasaidia wahusika wakuu kuendeleza riwaya. Wahusika hawa pia ni muhimu lakini mchango wao sio mkubwa kama wa wahusika wakuu. Tunagundua kuwa hata ingawa hawana mchango mkubwa kuweko kwao ni muhimu sana. Kwa mfano Mary Kasiva, huyu ni mamaye Susan.

Yeye haleti mgogoro wowote ambao ni sifa nzuri ya riwaya lakini yeye ndiye mlezi wa Susan aliye mhusika mkuu. Mary Kasiva anatekeleza vyema jukumu lake la malezi kwa watoto wakeakiwemo Susan mhusika mkuu wariwaya hii. Tuna wahusika kama mwalimu Birundu ambaye hata ingawa hana maadili mema ana jukumu nzuri la kufunza Susan shuleni. Wahusika hawa na wengine utafiti wetu ulipendezwa na mchango wao. Pia walifaa kuweko kama vile mwandishi alivyowachora.

Mwisho utafiti wetu umepata kuwa mandhari ya aina mbalimbali ambamo wahusika hawa wanaishi au kuyapitia, yaliwathiri kwa hali kubwa na wakaweza kuleta mchango mkubwa katika riwaya hii.

Utafiti huu umepata kuwa maisha ya Richard akiwa mjini yalikuwa magumu sana. Richard Ngunze alipokuwa mjini Nairobi kutafua kazi hakupata kazi maalum hivyo kupata riziki na kodi haikuwa rahisi. Hivyo hali hii ikamfanya kuamua kurudi nyumbani kujaribu bahati nyingine pale. Mandhari haya pia yaliweza kubadilisha maisha yake wakati alipata wahubiri fulani. Baada yake kusikiliza na kupata kama kungekuwa na matumaini katika dini aliamini na kuwa mkristo. Alipoenda nyumbani alishikilia msimamo huu. Tunamuona akiwa kiongozi kanisani na maisha yake yote kuwa mfuasi wa dini. Tunampata akipata riziki yake katika shamba alilokuwa nalo na pia kwenye huduma yake ya dini.

Maisha ya mjini pia yaliathiri maisha ya Mary Kasiva wakati alikuwa ameajiriwa na Manyara. Baada ya kupata mimba mhusika huyu alipoteza kazi na matumaini katika maisha. Kwa kuwa aliolewa akiwa na mimba ya mtu tofauti aliishi kwa hofu kuu kwa kuhofia siri yake ingegunduliwa na kumtia matatani.

Utafiti huu pia ulipata mandhari ya mashambani ilivyoathiri wahusika wa riwaya hii. Mandhari haya yalitumika kutoa mafundisho ya Biblia kwa watoto wa Richard. Ni nyumbani ambapo Richard alitoa mafundisho kwa wanao. Tulipata mafundisho haya yalimsaidia sana Susan shuleni kuamua mambo na kujipa moyo wakati wa shida. Tulimuona akikumbuka mafundisho na mashauri alipokuwa katika hali tofauti shuleni. Kwa mfano anakumbuka akishauriwa kujihadhari na wavulana, pia alipokuwa mgonjwa alikumbuka nguvu ya sala.

Tulipata kuwa hiki pia ni kipengelee muhimu sana riwayani. Mwisho katika sehemu hii tulipata mandhari ya shuleni. Mandhari haya yalimwathiri Susan kwa kiasi kikubwa. Baada ya kuona hali halisi ya mambo hasa alipokuwa chuoni alianza kudadisidadisi imani ya Richard babaye.

Baadaye alipata kuwa kulikuwa na udhaifu wa aina fulani. Ndipo akawa na ujasiri wa kumfichulia yaliyokuwa moyoni. Hali hii pia imefanya riwaya hii ipate mvuto mzuri. Hivyo utafiti huu umedhibitisha kuwa vipengele hivyo tumetaja vya fani vimeendeleza vyema maudhui ya kazi yote kwa njia iliyo mufti.

## 5.3 Hitimisho

Mwandishi wa riwaya ya *Nguvu Ya Sala* ametumia vipengele vya fani kwa ufundi wa hali ya juu. Ujumbe aliokusudia kuwasilisha umewasilishwa kwa njia inayoelewekakwa urahisi. Kupitia kwa vipengele vya fani, ujumbe wake unavutia na kuwa na kumpatia msomaji ari ya kusoma.

Vipengele vyenyewe ni kama vile msuko. Msuko ni moja wapo wa vipengele vilivyotumika kwa ufundi wa hali ya juu katika riwaya hii. Mwandishi ametumia wahusika kuupitisha ujumbe wake. Baadhi ya wahusika hawa ni wa kimviringo na wengine ni bapa. Hatimaye tumeshughulikia kipengele cha mandhari na kugundua namna mandhari tofauti yanavyoathiri wahusika na pia kudhibiti ujumbe.

## 5.4 Mapendekezo

Tulipendekeza vipengele vya fani tulivyotumia vitumike kupiumia uendelezaji wa maudhui katika kazi nyingine. Pia tungependekeza watafiti wa baadaye washughulikie kipengele cha kimtindo katika kazi za K.W. Wamitila na pengine kulinganisha na waandishi wengine.

## MAREJELEO


Brooks C.  na Warren R. P. (1943): *Understanding Fiction*. Fs Crofts & co., Inc.

Culler, J. (1975). *Structuralist Poetics: Structurelism, Linguistics and the Study of Literature:* London: Routledge and Kegan.

Forster E.M. (1927)*Aspects of the Novel.* London;Penguin Publisher

Njogu K. na Chimerah R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi. JKF.

Nkwera, F.M.V, (1978). *Sarufi na Fasihi:* Vyuo na Sekondari: Dar es Salaam: TPH.

Hornby A.S  (1978*): Oxford Student Dictionary of current English.* Hong Kong; Oxford University Press.

Kamera W.D na wenzake (1975): *Misemo na methali toka Tanzania*. Dar-es Salaam ;East African Literature Bureau.

King'ei K. na Ndalu A.  (2009*): Kamusi ya Semi*. Kampala; East African Educational Publishers Limited.

King'ei K. na Ndalu A. (2009): *Kamusi ya Methali.*East African Educational Publishers Limited. Kampala.

Mbatiah M. (2001): *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi.; Standard Textbook graphics and Publishing.

Mlacha, A.K na Madumulla J.S (1991): *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam ;University   Press. Dar es Salaam.

Msokile M. (1993). *Msingi wa Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publisher.

Murage J.N. (2011). *Uhakiki wa Fani katika Utendi wa Mwana Ninga.* Tasnifu ya uzamili Chuo kikuu cha Nairobi(Haijachapishwa.)

Murono E. na Andami A (2005) *Muundo Mpya Wa Methali*. Nairobi;Mvule Africa. Publishers.

Musyoka F.M. (1996). *Uhakiki wa Fani katika Tamthilia za Jay Kitsao* ,tasnifu ya uzamili Nairobi; Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Mwilaria R. (2011). *Fani katika Utenzi wa Ayubu.* Tasnifu ya uzamili Chuo kikuu cha Nairobi( haijachapishwa)

Ndungu N. (1996). *Uhakiki wa Fani katika Riwaya za Katama Mkangi* Tasnifu ya uzamili,Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi.(Haijachapishwa)

Saussure F (1974). *Course in General Linguistics.* London; Owen.

Senkoro F.E.M.K.. (1979). *Fasihi*, Press and Publicity Centre, Dar-es Salaam.

Syambo B. na Mazrui A. (1992): *Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi. East African Educational Publishers Ltd.

Wellek R. na Warren A. (1975). *Theory of Literature.* London; A Harvest/ HBJ Book

Tambasi P. ( 2011). *Uhakiki wa Fani katika Uteuzi wa Tambuka.* Tasnifu ya uzamili (haijachapishwa)

Too M.C. (2011). *Uchangamuzi wa Baadhi ya Fani katika Nguzo Mama.* Tasnifu bado ya uzamili (haijachapishw.)

Wamitila K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele Vyake.* Nairobi. Phoenix.

---------------- (2003): *Nguvu ya Sala.* Nairobi. Longhorn Publishers Ltd

----------------. (2007). *Mwenge wa Uandishi:* Nairobi. Vide-Muwa.

---------------- (2009). *Sesurumbe: Vito Vya Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa.

----------------- (2011): *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi. Focus Publishers

----------------- (2013): *Kamusi ya Misemo na nahau*. Longhorn Publishers. Nairobi